

**TOFAUTI ZA MSAMIATI BAINA YA KISWAHILI CHA MICHEWENI NA
KISWAHILI SANIFU**

TAREHE KHAMIS HAMAD

**TASINIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKIDHI SEHEMU YA
MASHARTI YA KUTUNUKIWA SHAHADA YA UZAMILI YA KISWAHILI
(M.A KISWAHILI) YA CHUO KIKUU HURIA CHA TANZANIA**

2018

UTHIBITISHO

Aliyetia sahihi hapa chini anathibitisha kuwa amesoma Tasnifu hii iitwayo “**Tofauti za Msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu**” na kupendekeza ikubaliwe na chuo Kikuu Cha Tanzania kwa ajili ya kukamilisha masharti ya shahada ya uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania

.....

Dr. Nestory N. Ligembe

(Msimamizi)

Tarehe

HAKIMILIKI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupiga chapa au kutoa baadhi ya maandishi ya kitabu hiki, kwa namna yoyote bila idhini ya mwandishi au Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania kwa niaba.

TAMKO LA MTAHINIWA

Mimi, **Tarehe khamis Hamad**, natamka na kuthibitisha kwamba tasnifu hii inayoitwa “**Tofauti za Msamiati Bainya ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu**” ni kazi yangu. Tasnifu hii haijawahi kuwasilishwa kwa lengo la kutunukiwa shahada ya uzamili au shahada nyingine yeoyote katika chuo kikuu kingine.

.

Saini**TAREHE KHAMIS HAMAD****Tarehe**

TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabruku kwa mume wangu Tahir, watoto wangu Muhsin, Yussuf na Mbarouk. Aidha, ninaitabaruku kwa marahemu baba yangu Bwana Khamis na mama yangu bibi Chumu Omar kwa malezi bora waliyonipa na kunisomesha mpaka nikafikia hapa nilipo.

SHUKURANI

Shukrani zangu za dhati ziende kwa Mwenyezi Mungu ambaye amenipa uhai na uzima wa afya pamoja na ustahamilivu wa hali ya juu na kuniwezesha kwa nguvu zote nikamilishe kazi hii ya utafiti. Shukrani nyingine zimwende mwingu wa rehma Mtume Muhammad (S.A.W). Kazi ya utafiti kwa yejote aliywahi kuifanya atakubaliana nami kwamba si kazi nyepesi kama wanavyodhania wengine, kwa sababu misaada ya watu mbali mbali ya hali na maliinahitajika katika kuchangia utafiti, vinginevyo unaweza ukashindwa na kukata tamaa kwa kile ulichokusudia kukamilisha. Nitakuwa mwizi wa fadhila nisiyekuwa na utu, kama sitowashukuru wale wote ambao wamenisaidia kwa njia moja ama nyingine katika kukamilisha kazi hii. Ingawa sitowataja wote kwa majina kwani si rahisi kuwataja wote ila kwa wale ambao sitowataja nawashukuru sana na waelewe kwamba mchango wao ulikuwa na manufaa kwangu ndio maana nikafikia hapa nilipo.

Pili natoa shukurani zangu za dhati kwa mwalimu wangu na msimamizi wangu wa utafiti huu, Dkt. Nestory N. Ligembe akiyenipa ushauri wa mara kwa mara na maelekezo hadi kukamilisha tasnifu hii. Sina cha kumlipa kutokana na yote aliyonifanyia katika kuhakikisha utafiti umekamilika kwa sababu wema alioufanya siwezi kuulipa ila namuombea kwa Mwenyezi Mungu ambariki kwa kumpa afya njema, uzima na mafanikio mema katika kazi zake.

Pia, natoa shukurani zangu kwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuniruhusu na kunibebea baadhi ya vipindi vyangu vya masomo ambavyo nilitakiwa niwe darasani kuvifundisha ili nikamilishe kazi hii. Aidha shukurani nyingine ziwaendee walimu na wanafunzi wa Skuli ya Wingwi Sekondari kwa kunipa

ushirikiano na kunielewa vizuri wakati wa harakati zangu za nmasomo. Hata hivyo shukran nyingine zimwende mwalimu Bakar Kombo kwa msaada, busara na ushauri aliotumia katika kipindi chote cha masomo ilhali nifanikishe kazi hii.

Naishukuru pia familia yangu wakiwemo mama mzazi bibi Chumu Omar na marehemu Bwana Khamis Hamad kwa malezi bora waliyonilea pamoja na kuwashukuru ndugu zangu Mchanga Khamis na Abubakar Khamis kwa msaada wao wa hali na mali . Sitomsahau mume wangu Bwana Tahir mbarouk na watoto wangu Muhsin, Yussuf na Mbarouk kwa ushirikiano niliopata kutoka kwao kwa kuwa wastahamilivu na wavumilivu jambo ambalo lilinifanya nisome kwa utulivu na matumaini.

Nawashukuru pia wanafuzni wenzangu wa shahada ya uzamilivu/umahiri katika Kiswahili kwa ushirikiano waliouonesha kwangu.

Mwisho nawashukuru wale wote walionipatia data kutoka maeneo ya Micheweni. Nyote nawaambia ahsanteni sana.

IKISIRI

Utafiti huu umelenga kuchunguza uhusiano uliopo baina ya tofauti za misamiati ya lahaja za Kipemba na zile za Kiswahili sanifu na jinsi tofauti hizo zinavyosababisha kukosekana kwa mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo na majedwali, sampuli iliyotumika ni sampuli rahisi. Eneo la utafiti ni Mkoa wa Kaskazini Pemba Wilaya ya Micheweni. Mbinu zilizotumika kukusanya data ni dodoso, usaili pamoja na mahojiano, kigezo cha umri na ukaazi kilizingatiwa kwa watoa taarifa. Nadharia ya isimu linganishi ndiyo iliyotumika katika kuchambua data iliyokusanywa. Matokeo ya utafiti huu yamebainisha kwamba kuna tofauti kubwa ya misamiati ya kilimo na misamiati inayotumika katika mazingira ya nyumbani kati ya lahaja ya Kipemba na Kiswahili sanifu hasa katika matamshi. Matokeo hayo yamedhihirisha kuwa ingawa kuna tofauti hizo, pia kuna uhusiano wa karibu wa maana ya misamiati hiyo yenye tofauti za matamshi na maumbo. Aidha matokeo hayo yamedhihirisha pia kwamba kwa kiasi fulani hali hiyo imesabababisha kukosekana mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji inayojitokeza kwa wazungumzaji wa Kiswahili cha Micheweni na wazungumzaji wa Kiswahili Sanifu. Mwisho utafiti huu unapendekeza kuwa wale wenye nia ya kuandika kuhusu isimu ya Kiswahili kwa kuchunguza maneno ya maeneo mbali mbaliya maeneo ya Kaskazini mwa kisiwa cha Pemba watumie matokeo ya utafiti huu kama mwongozo utakaowasaidia kuandika tafiti zingine. Hata hivyo, walimu na wanafunzi watumie tasnifu hii kama rejea ya kupata msamiati unaotumika katika Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Hata hivyo taasisi mbali mbali za lugha zihifadhi katika maandishi maneno ya Ki-Micheeweni na kuonesha wasemaji wa Ki-Micheweni wanazungumza Kiswahili cha kale kinachotofautiana kimatamshi na Ki-Sanifi

YALIYOMO

UTHIBITISHO	i
HAKIMILIKI.....	ii
TAMKO LA MTAHINIWA.....	iii
TABARUKU.....	iv
SHUKURANI	v
IKISIRI.....	vii
YALIYOMO.....	viii
ORODHA YA MAJEDWALI	xiv
ORODHA YA VIELEZO	xvi
ORODHA YA VIFUPISHO NA MAELEZO	xvii
SURAYA KWANZA.....	1

1.0 Utangulizi	1
1.1 Usuli wa Tatizo.....	1
1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti	2
1.3 Malengo ya Utafiti.....	3
1.3.1 Lengo kuu	4
1.3.2 Malengo mahsus.....	4
1.3.3 Maswali ya Utafiti	4
1.4 Umuhimu wa Utafiti.....	5
1.5 Mawanda ya Utafiti	5
1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake	6
1.7 Usanifu Wa Utafiti	6

1.8	Muhtasari wa Sura.....	6
SURA YA PILI.....		8
MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA KINADHARIA		8
2.1	Utangulizi	8
2.2	Mapitio ya Kazi Tangulizi.....	8
2.2.1	Misamiati ya Kiswahili cha Micheweni	12
2.2.2	Kiswahili Sanifu	12
2.2.3	Tofauti Bainya Misamiati ya Kiswahili cha Michewenina Misamiati ya Kiswahili Sanifu.....	13
2.2.3.1	Tofauti ya Wazungumzaji wa Luga Moja	14
2.2.3.2	Tofauti za Kitarafa.....	14
2.2.3.3	Tofauti za Kitabaka	15
2.2.3.4	Tofauti za Rejista.....	15
2.2.3.5	Tofauti za Lahaja.....	16
2.2.3.5.1	Lahaja za Kijiografia	16
2.2.3.5.2	Lahaja za Kijamii	17
2.3	Mapitio ya Tafiti za Kisayansi Zilizowahi Kufanyika	17
2.3.1	Msamiati wa Lahaja ya Kipemba cha Micheweni	18
2.3.2	Msamiati wa Kiswahili Sanifu	19
2.3.3	Athari za Kimawasiliano Zitokanazo Na Tofauti za Misamiati Bainya ya Lahaja ya Kipemba cha Micheweni na Kiswahili Sanifu	19
2.4	Kiunzi cha Nadharia.....	21
2.5	Muhtasari wa Sura.....	23

SURA YA TATU.....	24
MBINU NA NJIA ZA UTAFITI.....	24
3.1 Utangulizi	24
3.2 Muundo wa Utafiti	24
3.3 Eneo ya Utafiti.....	25
3.4 Walengwa wa Utafiti.....	26
3.5 Usampulishaji	26
3.6 Mbinu za Kukusanya Data	27
3.6.1 Mbinu ya Usaili	27
3.6.2 Mbinu ya Dodoso	28
3.6.3 Mbinu ya Maktaba.....	28
3.6.4 Mbinu ya Ushuhudiaji	29
3.7 Vifaa vya Utafiti	29
3.8 Mbinu ya Uchambuzi wa Data	29
3.9 Muhtasari wa Sura.....	30
SURA YA NNE.....	31
UWASILISHAJI WA DATA MATOKEO NA MAJADILIANO.....	31
4.0 Utangulizi	31
4.1 Data iliyokusanywa	32
4.1.1 Tofauti katika Shughuli za Kilimo	32
4.1.2 Tofauti katika mboga na Dawa za Majani.....	34
4.1.3 Tofauti katika Mazao.....	36
4.2 Msamiati wa Nyumabani.....	36

4.2.1	Tofauti ya Msamiati Unaotumika katika Mazingira ya Nyumbani.....	37
4.2.2	Tofauti zinazotokana na vifaa	37
4.2.3	Tofauti zinazojitokeza katika Maeneo.....	39
4.2.4	Tofauti zinazotokana na nomino za maradhi.....	40
4.2.5	Tofauti katika Vitenzi vya kawaida.....	41
4.2.6	Tofauti Katika Viulizi.....	43
4.2.7	Tofauti Katika Nomino.....	45
4.2.8	Tofauti Katika Nomino za Ki-Micheweni na Ki-Sanifu Zenye Asili ya Lugha za Kigeni	46
4.2.9	Tofauti za Majina ya Wadudu	48
4.2.10	Tofauti ya Majina ya Ukoo.....	49
4.2.11	Tofauti za Misamiati Inayohusu Vyakula	50
4.2.12	Tofauti Zinazojitokeza Katika Matamshi	52
4.3	Athari za Kimawasiliano Zitokanazo na Tofauti za Msamiati Bainya Ki- Micheweni na Ki-Sanifu	53
4.3.1	Mfumo wa Sauti	53
4.3.2	Irabu.....	53
4.3.3	Konsonanti.....	55
4.3.4	Viyeyusho.....	56
4.3.5	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti	57
4.3.6	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [gh]:[h].....	57
4.3.7	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [dh]: [z]	58
4.3.8	Tofauti ya Mabadiliko ya Fonimu [m] kuwa [n].....	59
4.3.9	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [j]: [z].....	61

4.3.10	Tofauti za Mabadiliko ya Sauti [z] kuwa [v].....	62
4.3.11	Tofauti ya mabadiliko ya sauti [ch] kuwa [sh]	63
4.3.12	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [sh] kuwa [s]	64
4.3.13	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [s] kuwa [sh]	65
4.3.14	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [th] kuwa [s]	66
4.3.15	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [l] kuwa [ly]	67
4.3.16	Tofauti ya mabadiliko ya Sauti [j]: [Ø]	68
4.3.17	Tofauti za ukaakaishaji wa sauti.....	69
4.3.18	Tofauti za Udondoshaji wa Udondoshaji wa irabu/fonimu.....	70
4.3.19	Tofauti katika Uchopekaji	72
4.3.20	Tofauti Inayojitikeza katika Mpumuo	74
4.3.21	Tofauti za Mifuatano ya Irabu	75
4.3.22	Tofauti za Maneno yenye Kuambatana	76
4.3.23	Tofauti Zinazojitokeza katika Maneno ya Urudufishaji.....	77
4.3.24	Tofauti Zinazotokana na Lafudhi	78
4.4	Matokeo ya Utafiti.....	80
4.4.1	Tofauti za Msamiati Unaohusu Shughuli za Kilimo Unaotofautina baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu	80
4.4.2	Tofauti ya Msamiati wa Nyumbani, Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu.....	81
4.2.3	Athari za Kimawasiliano za Fonolojia Msamiati wa Kiswahili Sanifu na Kimicheweni	81
4.3	Muhtasari wa Sura.....	82

SURA YA TANO.....	83
MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPEDEKEZO	83
5.0 Utangulizi	83
5.1 Muhtasari wa Utafiti.....	83
5.2 Hitimisho	86
5.3 Mapendekezo.....	87
BIBLIOGRAFIA.....	88
VIAMBATANISHO.....	90

ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali la 2.1	Tofauti za msamiati baina ya Ki-micheweni na Ki-sanifu	12
Jedwali la 2.2.	msamiati wa Ki-Sanifu	13
Jedwali la 4.1:	Tofauti ya Msamiati Katika Shughuli za Kilimo.....	32
Jedwali la 4.2:	Tofauti Zitokanazo na Mboga na Majani na Dawa za Watoto za Majani.....	35
Jedwali la 4.3:	Tofauti Katika Mazao.....	36
Jedwali la 4.4:	Tofauti Zinazotokana na Vifaa	38
Jedwali la 4.5:	Tofauti zinazojitokeza katika maeneo	39
Jedwali la 4.6:	Tofauti za Misamiati Kuhusu Maradhi.....	40
Jedwali la 4.7:	Tofauti katika Vitenzi vya Kawaida	41
Jedwali la 4.8:	Tofauti katika Viulizi.....	43
Jedwali la 4.9:	Tofauti Katika Vivumishi.....	44
Jedwali la 4.10:	Tofauti Katika Nomino za Ki-Micheweni na Ki-Sanifu Yenye Asili ya Kibantu	46
Jedwali la 4.11:	Tofauti za Nomino Zenye Asili ya Lugh za Kigeni.....	47
Jedwali la 4.12:	Tofauti za Majina ya Wadudu	48
Jedwali la 4.13:	Tofauti za Majina ya Ukoo.....	49
Jedwali la 4.14:	Tofauti za Misamiati Inayohusu Vyakula	51
Jedwali la 4.15.	Irabu Katika Ki-Sanifu	54
Jedwali la 4.16:	Irabu Katika Ki-Micheweni.....	55
Jedwali la 4.17:	Tofauti za Mabadiliko ya Sauti [gh] : [h].	58
Jedwali la 4.18:	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [dh]: [z]	59
Jedwali la 4.19:	Tofauti ya Mabadiliko Fonimu [m] Kuwa [n].....	60

Jedwali la 4.20:	Tofauti ya Mabadiloko ya Sauti [j]Kuwa [z].....	61
Jedwali la 4.21:	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [z] Kuwa [v].....	62
Jedwali la 4.22:	Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [Ch] kuwa [Sh]	63
Jedwali la 4.23:	Tofauti Za Mabadiliko Ya /Sh/ - /S/	64
Jedwali la 4.24:	Tofauti za Mabadiliko ya [S]-Kuwa [Sh]	65
Jedwali la 4.25:	Tofauti Ya Sauti [Th] Kuwa [S]	66
Jedwali la 4.26:	Tofauti Ya Sauti [L] Kuwa [Ly].....	67
Jedwali la 4.27:	Tofauti Ya Sauti [J] Kuwa [Ø]	68
Jedwali la 4.28:	Tofauti Za Ukaakaishaji Bainya Ki-Micheweni Na Ki-Sanifu.....	69
Jedwali la 4.29:	Udondoshaji Wa Irabu/Fonimu	71
Jedwali la 4.30:	Tofauti Katika Uchopekaji[Y].....	72
Jedwali la 4.31	Tofauti katika Uchopekaji [w].....	73
Jedwali la 4.32:	Tofauti katika Mpumuo	74
Jedwali la 4.33	Tofauti Katika Mfuatano wa Irabu	75
Jedwali la 4.35:	Tofauti ya Maneno ya Urudufishaji.....	78
Jedwali la 4.36	Tofauti Zinazotokana na Lafudhi	79

ORODHA YA VIELEZO

Kielelezo cha 3.1:	Ramani ya eneo la utafiti:	25
Kielelezo cha 4.1 :	Irabu Msingi za Lugha za Ki-Sanifu.....	54
Kielelezo cha 4.2.	Konsonanti	56

ORODHA YA VIFUPISHO NA MAELEZO

Ki	Sanifu : Kiswahili Sanifu.
Ki-	Micheweni : Kiswahili kinachozungumzwa Micheweni.
Viswahili hivi:	Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu.
Pande hizo mbili:	Upande wa wasemaji wa Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.
KS	Kiswahili Sanifu.
KM	Kiswahili cha Micheweni
Uk.	Ukurasa.
N.k.	Nakadhalika.

SURAYA KWANZA

1.0 Utangulizi

Sura hii imegawanyika katika Sehemu ya kwanza imejadili usuli wa tatizo. Katika sehemu hii imeeleza kwa undani namna waandishi mbali mbali pamoja na tafiti nyingine kuhusu lugha na lahaja za Kiswahili zilizofanywa katika mwambao wa Afrika Mashariki. Sehemu ya pili imeeleza tatizo la utafiti, ambapo mtafiti ameeleza tatizo litakalofanyiwa utafiti likiwa ni tofauti za msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu. Sehemu ya tatu inatoa maelezo kuhusu malengo ya utafiti likiwemo lengo kuu na malengo mahsusini pamoja na maswali ya utafiti. Sehemu ya nne ya sura hii inatoa maelezo kuhusu umuhimu wa utafiti. Pia sehemu ya tano inaelezea mawanda ya utafiti kwa kina. Sehemu ya sita ya sura hii inaeleza vikwazo vya utafiti na utatuzi wake. Mwisho sehemu ya saba, inatoa muhutasari wa sura nzima ya kwanza.

1.1 Usuli wa Tatizo

Zipo tafiti mbali mbali zilizokwisha fanywa za kuchunguza tofauti za usemajii wa lugha katika kisiwa cha Pemba na kuonesha kuwa wasemaji hao wanaweza kutofautiana kimatamshi, na hata maana kwa baadhi ya misamiati kutoka eneo moja hadi jingine. Baadhi ya wataalamu waliochunguza tofauti ya Kiswahili sanifu na Ki-Pemba ni pamoja na Kipacha, (2002), Khamis, (1984) na Masebo na Nyangwine (2004) na wengine. Wataalamu hawa wamebaini kuwa Kiswahili kizungumzwacho katika Kisiwa cha Pemba kinatofautiana kimatamshi na kimsamiati. Hali hii tunaweza kuiona kupitia wazungumzaji wa mjini na vijiji, kuwa Kiswahili kizungumzwacho Wete ni tofauti na kile cha Micheweni. Vile vile Kiswahili

kzungumzwacho Micheweni ni tofauti na kile kzungumzwacho Chake-chake. Ushahidi huu unaonekana kupitia kauli ya Massamba (2007:71) kwamba, *Ukienda Pemba kwa mfano Kiswahili kzungumzwacho Micheweni ni tofauti na kile kzungumzwacho katika kisiwa cha Kojani.*

Maelezo hayo yanamaanisha kuwa matamshi hutofautiana kutoka eneo moja hadi lingine ingawa hakuna uchunguzi wa kina ambao umefanywa wenyewe malengo ya kuonesha tofauti hizo za kifonolojia. Baadhi ya watafiti wakiwemo Khamis, Kipacha (wameshatajwa) walichunguza tofauti ya msamiati baina ya miji na vijiji kiujumla wake bila kubainasha namna gani matamshi ya Kiswahili cha maeneo ya vijijini na mjini yanatofautiana. Kazi za wataalamu mbali mbali akiwemo Khamis (keshatajwa) ziligusia tofauti za msamiati kati ya Kipemba cha mjini na cha vijijini, lakini katika uchunguzi wake alilinganisha isimu kwa ujumla. Kutokana na hali hiyo utafiti huu umechunguza tofauti za msamiati wa Kiswahili cha Micheweni (KM) na Kiswahili sanifu (KS). Lengo ni kuweka wazi namna ambavyo tofauti hizo zinabainika kupitia fonolojia ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu katika msamiati.

1.2 Tamko la Tatizo la Utafiti

Ipo shaka ya kuwa kuna tatizo la kutofanyika mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa Kiswahili cha Micheweni na wale wanaoongea Kiswahili sanifu.(Juma,20011; Abdalla, 2012). Misamiati ya Kiswahili cha Micheweni Kisiwani Pemba kinachozungumzwa katika baadhi ya maeneo ya kisiwa hicho inatofautiana kwa kiasi kikubwa na ile ya Kiswahili sanifu. Jambo hilo ni moja ya mambo yanayofikiriwa kukwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa lugha ya Kiswahili sanifu na wazungumzaji wa Kiswahili cha Micheweni. Jambo

lingine linalofikiriwa kukwamisha mawasiliano fanisi baina ya wazungumzaji wa makundi haya mawili ni matamshi ya vitamkwa vyta misamiati ya Kiswahili. Tofauti iliyopo baina ya misamiati hiyo inadaiwa kuwa inaweza kuwa chanzo cha mzungumzaji wa Kiswahili cha Micheweni Kisiwani Pemba kushindwa kuyaelewa mazungumzo ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu. Mfano, mzungumzaji wa Kiswahili cha Micheweni akisema UNANIFAHAMU akiwa na maana ya UNANIELEWA, si rahisi kwa masemaji wa Kiswahili sanifu kuifasili haraka maana yake sahihi.

Hata hivyo hakuna uchunguzi uliofanywa wa kuchunguza athari ya tofauti hizi kwa wazungumzaji wa Kiswahili cha Micheweni katika visiwa vyta Pemba. Kutokana na upungufu huo kumekuwa na pengo kubwa la kufanya utafiti utafiti wa kina juu ya athari ya tofauti hizi za kimsamiati baina ya wazungumzaji wa makundi haya mawili katika mawasiliano ya kila siku. Utafiti huu umechunguza tofauti baina ya misamiati ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu na jinsi tofauti hizo zinavyoathiri mawasiliano baina ya makundi ya wazungumzaji wa lugha hizo. Utafiti huu umechunguza tofauti baina ya misamiati ya shughuli nyingi za kijamii kama vile kilimo na shughuli za nyumbani. Utafiti umechunguza tofauti baina ya misamiati hii kwa kuzingatia aina mbali mbali za maneno kama vile vitenzi, vivumishi, viulizi, nomino n.k.

1.3 Malengo ya Utafiti

Adam na mwenzake (2008) wanasema kuwa malengo ya utafiti ni yale madhumuni yaliyokusudiwa na mtafiti. Malengo hutueleza mtafiti anataka kupata nini mwisho wa utafiti wake. Malengo ya utafiti ni malengo makuu na malengo mahsus.

1.3.1 Lengo kuu

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza tofauti baina ya misamiati ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu na jinsi tofauti hizo zinavyoathiri mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lugha hizo.

1.3.2 Malengo mahsusini

Katika kufikia lengo kuu la utafiti huu, mtafiti wa kazi hii atajishughulisha na malengo mahsusini yafuatayo:

- i. Kubainisha misamiati ya lahaja ya Kipemba cha Micheweni itokanayo na shughuli na kilimo pamoja na mazingira ya nyumbani inayotofautiana na ile ya Kiswahili Sanifu.
- ii. Kubainisha athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu.

1.3.3 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu umetoa majibu ya-mawsali yafuatayo:

- i) Ni misamiati ipi ya lahaja ya Kiswahili cha Kipemba cha Micheweni unaotumika katika shughuli za kilimo na shughuli za matumizi ya nyumani inayotofautiana na ile ya Kiswahili sanifu?
- ii) Ni athari gani za kimawasiliano zinazojitokeza kwa wazungumzaji wa makundi haya mawili kutokana na tofauti za kimsamiati baina ya lahaja ya Kipemba cha Micheweni na Kiswahili Sanifu?

1.4 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utakuwa una umuhimu mkubwa katika mgawanyo wa lahaja na matumizi ya lugha ya Kiswahili. Utafiti huu unajibainisha katika vipengele vifuatavyo:

Utafiti huu utakuwa muongozo kwa wale wanaotarajia kuandika kuhusu tofauti za msamiati wa Kiswahili cha Pemba cha Micheweni na Kiswahili sanifu.

Pia utakuwa dira kwa watunga sera ambao wanatarajia kuimarisha nakuendeleza lahaja za Kiswahili.

Aidha utafiti huu utachangia katika taaluma kwa kuhifadhi maneno ya Kiswahili cha Micheweni yanavyotofautiana na Kiswahili sanifu katika maandishi na matamshi.

Vile vile utafiti huu utaamsha ari kwa wasomi wengine wa isimu na lugha kufanya tafiti nyingine zinazohusiana na tofauti za misamiati katika matamshi ya Kiswahili sanifu na maeneo mengine.

Utafiti huu pia utakuwa marejeleo na msaada kwa walimu na wanafunzi wengine wa lugha katika taaluma ya kujua tofauti ya matamshi ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu.

1.5 Mawanda ya Utafiti

Utafiti huu kimsingi umeweka wazi tofauti za kimsamiati katika matamshi ya Kiswahili sanifu na Kiswahili cha Micheweni na haukuingia katika kipengele cha mofolojia na sintaksia kwa sababu hayakua katika malengo ya utafiti huu. Vipengele vingine vinaweza kujadiliwa katika tafiti zingine. Hata hivyo, si kwamba vipengele hivyo havikutumika moja kwa moja katika utafiti huu bali vimeweza kutumika pale ambapo imestahiki ili kubainisha na kutoa taarifa zaidi.

1.6 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi wake

Katika utafiti huu kumejitokeza changamoto au vikwazo vifuatavyo:

Baadhi ya watafitiwa kutokuwa tayari kutoa msamiati wa maeneo ambamo wanaishi. Hivyo mtafiti alitafuta watu wengine ambao walikuwa tayari kumpatia taarifa kwa ridhaa yao.

Tatizo katika upatikanaji wa maana au uelewa wa baadhi ya msamiati ambao ulitolewa na watafitiwa. Mtafiti ili kuondoa usumbufu alitafuta mtu au watu wanaoelewa vyema maana ya misamiati hiyo katika Kiswahili sanifu.

1.7 Usanifu Wa Utafiti

Taarifa za matokeo ya utafiti zimewasilishwa na kuchambuliwa katika tasnifu ambayo ina sura tano, kila sura imekuwa na kipengele kinachojitegemea. Sura ya kwanza imekuwa na utangulizi, sura ya pili imekuwa na mapitio ya kazi tangulizi, sura ya tatu ni mbinu na njia za utafiti, sura ya nne ni uwasilishaji na uchanganuzi wa data sura ya tano ni matokeo, mapendekezo na hitimisho la utafiti. Kila sura imeanza na utangulizi katika mpangilio wa tasnifu na kufuatiwa na kipengele ambavyo vimewasilishwa kwa nambari. Mwisho wa kila sura kuna muhtasari ambao umeonesha ufupisho wa kila sura.

1.8 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii tumeeleza namna waandishi mbali mbali pamoja na tafiti nyingine kuhusu lugha na lahaja za Kiswahili. Pia tatizo la utafiti, ambapo mtafiti ameeleza tatizo litakalofanyiwa utafiti ambalo ni tofauti za msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu. Hata hivyo kipengele kingine cha sehemu hii

kinatoa maelezo kuhusu malengo ya utafiti yakiwemo malengo makuu na malengo mahsus i pamoja na maswali ya utafiti. Sehemu ya nne ya sura hii inatoa maelezo kuhusu umuhimu wa utafiti. Pia sehemu ya tano inaelezea mawanda ya utafiti kwa kina. Na sehemu ya sita ya sura hii inaeleza vikwazo vyta utatuzi wake

SURA YA PILI

MAPITIO YA KAZI TANGULIZI NA KIUNZI CHA KINADHARIA

2.1 Utangulizi

Sura hii imegawika katika vipengele vikuu vitatu, kipengele cha kwanza kimefanya mapitio ya kinadharia. Katika kipengele hiki maelezo bayana juu ya mitazamo mbalimbali kuhusu lahaja za Kiswahili cha Kipemba yametolewa na wataalamu wa utafiti. Kipengele cha pili kimejadili kwa kirefu tafiti mbalimbali zilizofanyika juu ya lahaja za Kiswahili katika Kisiwa cha Pemba. Sehemu ya tatu imeangalia kiunzi cha nadharia kilichomuongoza mtafiti katika uchanganuzi wa data. Na sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura yote.

2.2 Mapitio ya Kazi Tangulizi

Kazi mbali mbali zimekwisha fanywa na baadhi ya wataalamu wakiwemo wageni na wenyeji ili kuchunguza baadhi ya lahaja za Kiswahili. Waanzilishi wakiwa ni wageni walifanya juhudhi ya kuangalia namna lugha zinavyofanana ama kutofautiana katika vipengele mbali mbali vikiwemo msamiati. Wataalamu hao kama ambavyo Kipacha (2003) anasema, kazi ya mwanzo ya utafiti wa lahaja iliandikwa mwanzoni mwa karne ya 19 ili kuweza kufahamu lugha za wenyeji wa Pwani na kurahisisha shughuli za uenezaji wa dini na utawala. Baadhi ya lahaja zilizochunguzwa na wataalamu hao ni kama vile, Kimtang'ata (Whitely, 1958), na Ingrams (1942) analinganisha lahaja mbali mbali za Kiswahili zinazozungumzwa katika visiwa vyta Zanzibar yaani Kipemba, Kihadimu, Kitumbatu na Kiunguja Mjini. Katika uchunguzi wake alibainisha kuwa:

*....Wapemba wanazungumza lahaja moja.....
inayoitwa Kipemba, inatofautiana vile vile na
Kihadimu na Kitumbatu*

Kazi ya Ingrams inalinganisha msamiati wa lahaja hizo bila kuangalia vipengele vingine vyta kiisimu katika maeneo mbali mbali yaliyomo ndani ya lahaja moja. Pengo la kazi nikuwa hakuangalia athari gani za kifonolojia katika misamiati zinazotofautiana kati ya lahaja ya Kipemba cha Micheweni na Kiswahili sanifu. Whitely (1958) alichunguza ushairi wa Kiswahili cha Pemba na akagundua kuwa katika kisiwa cha Pemba kuna lahaja tofauti zinazozungumzwa katika maeneo tofauti. Mfano eneo la Micheweni –Wingwi (Kaskazini Mashariki ya Kisiwa), Kisiwa cha Kojani (Mashariki), na Matale (Kusini ya Kojani) na alifanya uchunguzi wa kiisimu. Ingawa aliyagusia maeneo tofauti katika kazi yake lakini maeleo yake hayatoshelezi kuonesha uchambuzi wa kiisimu wa tofauti za Kiswahili kizungumzwacho maeneo mbali mbali ya Kisiwa cha Pemba.

Mtaalamu mwengine ni Sacleus (1909) ambaye pia anazungumzia kuhusu lahaja ya Kipemba kuna lahaja ndogo nne, ambazo ni kama vile:

*Kipemba cha Kusini, Kipemba cha Kivitongoji
(mvumoni), Kichake- Chake na Kimsuka Chalen*

Katika uchunguzi wake anaeleza matumizi ya kiambishi **ki-** kinachozungumzwa katika Kipemba badala ya **ch**-mfano huu unajitokeza katika neno kyombo kyema badala ya chombo chema. Hata hivyo, kazi yake haikuonesha uchambuzi wa kina kuhusu tofauti za msamiati wa lahaja alizozia inisha.

Kwa upande wa Kipacha (2003) naye alifanya tafiti mbali mbali kuhusu lahaja za Kiswahili zinazopatikana Mwambao wa Afrika Mashariki kama vile Kitikuu, Kitumbatu, Kimvita, Kiamu, Kipate, Kimrima, Kisiu, Kipemba, Kiunguja n.k. Katika utafiti wake alibainisha tofauti zilizopo kati ya lahaja moja na Kiswahili sanifu kwa kuangalia msamiati, fonolojia na baadhi ya vipengele vya kiisimu katika lahaja ya Kipemba. Ingawa alifanya juhudini kubwa ya uchambuzi wa lahaja ya Kipemba lakini hakubainisha uchambuzi huo namna unavyojoitokeza katika eneo moja na jingine la Kisiwa cha Pemba.

Katika utafiti huo tumegundua kuwa baadhi ya maneno ambayo ameyaweka katika kazi yake hayana maana halisi kama yanavyotumiwa na Wapemba. Mfano neno ‘kisingano’ lenye maana ya kisigino, ‘kisusi’ lenye maana ya ukuta, ‘fisa’ lenye maana ya tuma na mengineyo.

Hata hivyo mwishoni mwa karne ya 19 waliibuka wazawa ambao waliunga mkono juhudini zilizofanywa na wageni hao na kutafiti lahaja za Kiswahili. Miiongoni mwao ni Temu (1980), Batibo (1982), Khamis (1984), Mshindo (1989). Wataalamu hawa katika tafiti zao waliangalia vipengele vya sarufi za lahaja hizo kwa kulinganisha vipengele hivyo na vya Kiswahili sanifu badala ya kulinganisha ama kutofautisha usemaji wa eneo moja na jingine.

Polome (1967) katika utafiti wake anaendelea kusema kuwa

*Kipemba kinazungumzwa katika kisiwa cha Pemba
ispokua Pemba Kusini ambako hakuna ukaakaishaji
wa kiambishi ki-kabla ya nomino zinazoamza na
irabu. Katika baadhi ya maeneo kama vile Micheweni
–Wingwi, pembae ya kaskazini lahaja ndogo*

zimetokea. Mfano Micheweni wanatumia 'k' badala ya 'h' katika kiambishi cha ukarusha nafsi ya pili au ya tatu umoja. (Tafsiri yangu).

Batibo (1982) naye alifanya utafiti wa kulinganisha lajaja za kisini za mwambao wa Afrika Mashariki. Baadhi ya maeneo aliyo tembelea ni Tanzania Bara na maeneo ya Unguja mjini. Katika utafiti wake ameona kuwa lajaja zote zinakaribiana. Kwa kusema:

...kufuatana na matokeo haya lajaja zote zinakaribiana kwa vile kwa ujumla hakuna tatizo katika kuwasiliana baina ya wazungumzaji wa lajaja zote.

Maelezo haya ya Batibo hayana ukweli kwani licha ya watu wanaozungumza Ki-Sanifu, watumiaji wa lajaja nyingine wanapata ugumu katika kuwasiliana kwao. Labda utafiti wake ulizingatia zaidi maeneo ya mjini na kusahau maeneo ya vijiji ambako hujitokeza tofauti za kiusemaj. Hivyo, utafiti wake hauna mchango katika utafiti huu.

Khamis (1984) alichunguza tofauti baina ya Kipemba kinachozungumzwa mjini na kile cha vijiji. Katika utafiti wake alichunguza tofauti mbali mbali za kiisimu. Ingawa uchunguzi wa Khamis ni wa kina lakini lakini hakufafanua baadhi ya vijiji na kuona tofauti au mfanano wa wazungumzaji hao wanaoishi eneo moja na jingine. Khamis anasema:

Tulijikita katika kutafiti maeneo ya mjini na baadhi ya vijiji vya ndani. Ni wazi kuwa uchunguzi unahitajika katika vijiji vingine... (tafsiri ni yangu).

Utafiti wa Khamis umetusaidia kupata data mbali mbali za kiisimu zinabainisha kupata tofauti za msamiati baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu

2.2.1 Misamiati ya Kiswahili cha Micheweni

Misamiati ya lajaja ya Kiswahili cha Micheweni ni maneno yote ambayo yanatumika katika shughuli mbali mbali za kijamii kama vile kilimo, uvuvi , biashara , siasa n.k. baadhi ya watafiti(Juma, 2011, Abdalla, 2012) wamegundua kwamba kuna tofauti za kiusemajji wa Kiswahili katika maeneo ya Micheweni ukilinganisha na Kiswahili sanifu. Tofauti hizo zinaweza kujitokeza katika msamiati unaotumika kama vile kuacha baadhi ya sauti katika usemajji, kuongeza sauti katika baadhi ya msamiati, kubadili herufi, kudondosha, kuunganisha maneno wakati wa uzungumzaji, kiimbo, ufupishaji wa maneno n.k. Katika baadhi ya maneno kama ambavyo jedwali linafafanua hapo chini:

Jedwali la 2.1 Tofauti za msamiati baina ya Ki-micheweni na Ki-sanifu

	Ki-micheweni	Ki-sanifu
Kubadili fonimu	Nchele	Mcchele
Kuongeza/kuchopeka	Hofisi	Ofisi
Kudondosha	Uyu	Huyu
Urefushaji wa maneno	Muungu	Mungu n.k

Chanzo: Mgullu (2001)

2.2.2 Kiswahili Sanifu

Kiswahili sanifu ni kile ambacho kinatumika katika shughuli zote rasmi kama vile ofisisni, mikutanoni, mahakamani, bungeni n.k. Misamiati ya Kiswahili sanifu ambayo itatumika katika utafiti huu ni ule unaotumia katika shughuli rasmi unaotofautiana na lajaja nyengine au lugha nyingine zisizokuwa rasmi. Kwa

kawaida msamiati wa Kiswahili sanifu umeepukana na athari za kifonolojia zinazojitokeza katika usemajii kama vile udondoshaji, uchopekaji, ubadilishaji wa sauti n.k. Baadhi ya misamiati hiyo ni kama vile:

Jedwali la 2.2. msamiati wa Ki-Sanifu

Msamiati	K/S
Mkate	Mkate
Huyu	Huyu
Ofisi	Ofisi.

Chanzo: Data za Uwandani 2016

2.2.3 Tofauti Bainya Misamiati ya Kiswahili cha Michewenina Misamiati ya Kiswahili Sanifu

Misamiati wa lahaja ya Kipemba cha Micheweni inatofautiana na misamiati wa Kiswahili sanifu. Tofauti hiyo inaonekana kuitia vipengele tofauti kama vile kiimbo, lafudhi, maumbo ya maneno, matamshi, mabailiko ya baadhi ya fonimu, udondoshaji wa baadhi ya vitamkwa n.k. Tofauti hii inaonekana kuitia mazungumzo ambayo yanatokana na wanajamii wa Micheweni unapoyalinganisha na yale ya Kiswahili sanifu.

Hivyo, baadhi ya wanavyuoni wa lahaja za lugha wakiwemo Mathooko, (2007), Gumpers, (1968) na Mdee, (2004). Wamebaini kwamba kuna kufanana na kutofautiana kwa lahaja hizo kwa kutumia kigezo cha kiisumu. Tofauti hizo zinaweza kujitokeza kwa wazungumzaji wa lugha moja, au tofauti za wazungumzaji za kitarafa au kitabaka.

2.2.3.1 Tofauti ya Wazungumzaji wa Lugha Moja

Kwa kuwa lugha ni zao la jamii na kwa kuwa ina mpangilio maalum unafuatwa na wana jamii husika ili iweze kutoa ujumbe lakini mpangilio huo pamoja na maana lazima kuwe na makubaliano mionganoni mwa wanajamii hao. Ndani ya jamii lugha moja watu hutofautiana katika utamkaji wa lugha hiyo kama ambavyo Mdee (2004) anasema: tofauti za lugha zinaweza kuwa kwa mujibu wa tofauti zao za kiuchumi, aina ya kazi wanayoifanya na hata eneo wanaloishi huweza kujidhihirisha katika msamiati au maneno wanayoyatumia na katika matamshi n.k. kwa mfano vijana wa vijiweni au wafugaji huwa na msamiati wao wanapokuwa katika kundi lao, watu wa eneo maalum pia huongea lahaja ya mahali pale na hata wakiwa nje ya eneo lao hutambulika kutokana na msamiati wanaoutumia na namna wanavyotamka ambavyo huwatambulisha mahali wanapotoka.

Gumperz (1968) akielezewa na Mathooko (2007) anaeleza kuwa kuitia jamii lugha watu wanatofautiana kwa ishara za kimaongezi katika matumizi yao ya lugha.

Mdee (keshatajwa) anaendelea kusema kuwa:

Tofauti za kiisimu kama vile kifonolojia, kisarufi, kimsamiati n.k. hubainisha vilugha/ lahaja ndani ya lugha moja. Hata hivyo anaeleza kuwa sababu za kutokea tofauti hizo zinaweza kuwa za kibinagsi, kitarafa, kitabaka, rejista au lahaja.

2.2.3.2 Tofauti za Kitarafa

Kwa mujibu wa Mdee (keshatajwa) ni kilugha cha wazungumzaji wa lugha ambao ni wa tabaka fulani katika jamii ambao hujibagua kulingana na nafasi zao. Hivyo, tofauti hizo za kijografia huchangia kuzuka kwa tofauti za kimatamshi au kimsamiati

ambazo zinamtofautisha mzungumzaji wa kitarafa kimoja na kingine ndani ya jamii lugha moja. Tofauti hizo zinapojitokeza mzungumzaji wa kitarafa kimoja inakuwa vigumu kuelewa au kufahamu kinachozungumzwa na mzungumzaji wa kitarafa kingine.

2.2.3.3 Tofauti za Kitabaka

Nitofauti za uzungumzaji zinazojitokeza kutokana na kuwepo kwa matumizi tofauti ya wazungumzaji wa kila tabaka lililopo ndani ya jamii k.v. tabaka la juu na tabaka la chini (wafanyakazi). Kipacha (2003) anasema kuwa tabaka la juu huzungumza zaidi lugha rasmi wakati lile la chini linatumia zaidi lafudhi yenyе taathira za vitarafa.

Mdee nae katika (2004) anazungumzia kitabaka kuwa ni kilugha kinachozungumzwa na watu wa tabaka fulani katika jamii ambao hujibagua kulingana na nafasi zao walizonazo ziwe kiuchumi, kisiasa au kielimu. Hivyo ndani ya jamii lugha moja kuna matabaka mbali mbali ambayo kwa njia moja au nyingine yanatofautiana kulingana na msamiati, ambao utatumwiwa na tabaka fulani au jingine.

2.2.3.4 Tofauti za Rejista

Rejista ni mtindo wa lugha unaotumika mahali penye shughuli fulani ambao ni tofauti na lugha ya kawaida kwa mfano lugha ya wavuvi, ya kihuni, ya kibiashara, nk.(Masebo na Nyangwine 2002). Pia, Mathooko (2007) anasema, Rejista ni mtindo wa lugha kutegemea na muktadha wa kijamii.

Hivyo, kimsingi rejista ni mtindo wa lugha unaotumika mahali penye shughuli fulani au kundi fulani lililomo ndani ya jamii ambayo ni tofauti na lugha ya kawaida.

2.2.3.5 Tofauti za Lahaja

Massamba (2004) anaeleza kuwa lahaja ni lugha moja wapo baina ya lugha ambazo kimsingi huhesabiwa kuwa lahaja moja isipokuwa zinatofautiana katika mambo madogo kama lafudhi au msamiati usio wa msingi. Tofauti hizo anazifafanua katika matamshi kupitia kazi yake ya (2007:71) kwa kusema kuwa Ukienda Pemba kwa mfano Kiswahili kinachozungumzwa Micheweni ni tofauti na kile kinachozungumzwa katika kisiwa cha Kojani.

Aswami na wenzake (2006) anaifasili lahaja kuwa ni vilugha vidogo vidogo vyta lugha moja. Anaendelea kusema kuwa lahaja ni aina moja ya lugha inayojisimamia katika misingi ya kijamii au kijimbo. Lahaja zinaweza kufanana na kutofautiana katika matamshi, muundo wa kisarufi na msamiati kulingana na eneo la kijiografia linalotenganishwa na vilima na visiwa.

Hivyo tunaweza kusema kuwa lahaja ni tofauti za kimsamiati, kimatamshi na kisarufi ambazo hujitokeza katika ligha kuu kutokana na tofauti za kijiografia katika eneo husika. Tofauti hizo hupelekea watu wa eneo moja au kundi moja kutengwa kimawasiliano na kundi jingine au watu wa eneo jingine. Kulingana na maelezo hayo tunaweza kuzigawa lahaja katika makundi mawili, ambayo ni lahaja za kijiografia na lahaja za kijamii (Kipacha, 2003; Mathooko, 2004).

2.2.3.5.1 Lahaja za Kijiografia

Ni lahaja ambazo wazungumzaji hutofautiana kwa kutenganishwa na mambo ya kimaumbile kama vile bahari, mito na milima. (Kipacha-amekwishatajwa)

anaendelea kusema kuwa iwapo watu wametenganishwa na visiwa, dini au itikadi inaweza kupelekea pia kuwa tofauti za lahaja.

Aswami (keshatajwa) anasema kuwa lahaja ni mgao lugha ambao unatokana na vizuizi vyta kiografia hususan milima, mito, ziwa, majangwa au hata upana wa eneo la lugha. Mfano wa lahaja hizo katika Kiswahili Chimiini, Ki-Mvita, Ki-Unguja, Ki-Pemba, Ki-Hadimu na nyenginezo.

Kutokana na maelezo hayo tunaona kwamba lahaja za kijiografia ni aina ya lahaja ambayo wazungumzaji hutofautiana katika matamshi, au msamiati kutokana na vizuizi vyta bahari, milima, mito au majangwa.

2.2.3.5.2 Lahaja za Kijamii

Kwa mujibu wa Aswami (Keshatajwa) anasema kuwa lahaja jamii ni tofauti za mgawanyo wa lugha ambao hautegemei vizuizi vyta kijiografia au kimaeneo. Tofauto zinaweza kuwa za kitabaka, elimu, jinsia au umri.

2.3 Mapitio ya Tafiti za Kisayansi Zilizowahi Kufanyika

Katika sehemu hii tafiti zilizowahi kufanyika ndani na nje ya nchi zenyet kufanana na utafiti huu ninaoufanya na maeneo ambayo hayakushughulikiwa na tafiti hizo zimeeleza kwa kina. Robinson (1981) anatoa maelezo kuwa lahaja ni kijilugha fulani kinachotumiwa na watu wachache ambacho humuwezesha msemajii wake kujipatia misamiati kutoka lugha ya asili, lakini kuna baadhi ya msamiati unaoweza kumueleza mtu anapotoka.

Kwa mfano, utafiti juu ya viangami ndani ya lahaja ya Kipemba vinavyokwamisha mawasiliano fanisi si tu kati ya Wapemba na wazungumzaji wengine wa Kiswahili sanifu na jinsi ambavyo lahaja ya Kipemba cha Micheweni inavyozungumzwa katika Wilaya ya Micheweni ina misamiati ya kipekee inayoweza kusababisha mzungumzaji wa lahaja nyingine za Kiswahili na Kiswahili sanifu kushindwa kuwasiliana kwa ufanisi . Kupitia vipengele hivyo tumeweza kuona kwamba wataalamu hao wakiwemo wa ndani na nje ya nchi wamechunguza kwa kina suala zima la tofauti za lahaja lakini hawakuangalia kwa undani kwamba ndani ya lahaja kuu kuna lahaja ndongondogo ambazo pia zinatofautiana na lahaja kuu katika kuleta ufanisi wa mawasiliano.

2.3.1 Msamiati wa Lahaja ya Kipemba cha Micheweni

Msamiati kwa mujibu wa Kaplon (2014) anasema msamiati ni maneno yanayotumika katika lugha fulani, ambao hujulikana kama maneno yasiyojulikana na watu wengi. Katika usemi huu ana maana kwamba msamiati unaweza kutofautiana kupitia maeneo tofauti ya wazungumzaji jambo ambalo linaathiri kupatikana kwa mawasiliano fanisi. Pia Khamis (keshatajwa) naye aliweza kuangalia msamiati wa kipemba cha Micheweni kiujuimla na kuona kuwa unaathiri mawasiliano kwa wale ambao si wakaazi wa Micheweni. Hivyo basi, ilionekana kwamba msamiati kupitia maeneo watu wanamoishi inaweza kutofautiana kwa njia moja au nyingine lakini haikuchunguzwa kwa kina vipi Kiswahili cha Micheweni hutofautiana na Kiswahili Sanifu. Kulingana na pengo hili ndipo tulipoangalia kwa kina tatizo lilikomsukuma mtafiti kufanya utafiti kwa kuangalia msamiati wa Ki-Micheweni.

2.3.2 Msamiati wa Kiswahili Sanifu

Mgulu (keshatajwa) anasema kuwa lugha sanifu ni nlugha ambayo imesanifishwa, na lugha inaposanifishwa vipengele vyote hushughulikiwa kama vile fonolojia , mfano wasanifishaji walikubaliana juu ya fonimu ambazo zitatumika kuunda maneno yte ya lugha pamoja na mpangilio wake na othografia. Vipengele vingine ni mofolojia, sintaksia na semantiki. Kulingana na maelezo haya Kiswahili ndicho kilichofanyiwa juhudhi hizo tangia miaka ya 1930 kwa kuunda kamati ya lugha ambayo iliteua kiunguja kitumike kama msingi wa Kiswahili sanifu. Tofauti iliyopo ni kwamba maneno ambayo yanazungumzwa katika Kiswahili sanifu yanaepukana na zile kasoro ndogo ndogo za kilahaja zinazokwamisha mawasiliano wakati Kiswahili cha Micheweni athari hizo zinajitokeza. Athazi hizo ni kama zile tulizozitaja zinazotokana na irabu na konsonanti.

2.3.3 Athari za Kimawasiliano Zitokanazo Na Tofauti za Misamiati Bainya

Lahaja ya Kipemba cha Micheweni na Kiswahili Sanifu

Tafiti mbalimbali zinaonesha kwamba lugha hutofautina kutoka eneo moja hadi jingine. Tofauti hizo zinaweza kuwa kupitia athari za mfumo wa sauti kama vile, irabu, konsonanti pamoja na viyeyusho. Katika tafiti hizo zimedhihirisha kwamba baadhi ya maeneo yanayozungumza lahaja kuu zipo lahaja nyingine ndogondogo zinazotofautiana kimatamshi kupitia vipengele hivyo kwani lugha au lahaja pia hutofautiana kupitia idadi ya sauti zitumikazo katika lugha hiyo. Baadhi ya tafiti hizo ni kama vile (Juma, 2011), Shaame, (2015) na Abdalla (2012) ambao katika kazi zao wamebainisha kuwa ingawa sauti zitumikazo katika lugha zinafanana na kutofautiana hata hivyo sauti hizo katika baadhi ya lahaja hupelekea kukosekana kwa

mawasiliano fanisi kwa wazungumzaji wanaozungumza lahaja tofauti zilizomo ndani ya lahaja kuu moja.

Irabu

Matinde (2012) anasema ni sauti ghuna ambayo hutamkwa bila mzuio wa hewa itokayo kwenye mapafu hadi kinywani. Wataalamu wengine wanaendelea kusema kwamba ni kitamkwa ambacho hutamkwa pasi na kizuizi chochote kile katika mkondo wa hewa utokao mapafuni kuitia katika chemba ya kinywa na chemba ya pua. (Masamba na wenzake, 2004). Kwa kuzingatia mahali zinapotoka irabu imebainika kwamba katika Ki-Micheweni irabu zake zinalinagana na zile za Ki-Sanifu ispokuwa athari inayojitkeza ni katika utamkaji jambo ambalo linaathiri upatikanaji wa mawasiliano kwa ufanisi. Ingawa tutafafanua zaidi katika uchambuzi wadata tunachotakiwa kuelewa ni kwamba katika KM kuna urefushaji wa irabu unaotofautiana na ule wa KS.

Konsonanti

Kwa mujibu wa kamusi la Kiswahili fasaha (2010) wanasema ni kitamkwa cha lugha kisichokuwa vokali

Kwa kuzingatia sifa ya mahali pa matamshi, konsonanti za Kisanifu huweza kuainishwa katika makundi mengine saba yaani, kuna konsonanti zenyе sifa ya: *midomo, midomo meno, ufizi meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini na koromeo*. Kimsingi ni kwamba konsonanti hizo katika viswahili hivi viwili hujitokeza athari ndogondogo zinazokwamisha mawasiliano kwa wazungumzaji wa viswahili hivyo.athari zenyewe zinanekana katika mabadiliko ya baadhi ya sauti. Katika KM

baadhi ya sauti zinabadilika na kuyafanya mawasiliano yawe magumu kwa wale ambao si wazawa wa maeneo hayo. Hivyo, hali inaonekana kupitia tafiti zilizopita kwamba tofauti ya maeneo ya watu wanamoishi iachangia kuwafanya wazungumzaji wa maeneo hayo kuweza kutofautina kimatamshi kama ambavyo wazungumzaji wa KM huengeza ama kupunguza baadhi ya sauti katika mazungumzo yao jambo ambalo ni tofauti katika KS.

2.4 Kiunzi cha Nadharia

Kwa mujibu wa Massamba (2002) Nadharia ni taratibu, kanuni na misingi ambayo imejengwa katika muundo wa kimaelezo kwa madhumuni ya kutumiwa kama kielelezo cha kueleza jambo. Kiunzi cha nadharia ambacho kitatumika katika utafiti huu ni kile cha nadharia ya Isimu linganishi.

Mgullu (2001) akimnukuu Lehman (1973) anelezea kuwa lengo mahususi la tawi hili la isimu huwa ni kufanya uchunguzi wa lugha mbali mbali ili kuzilinganisha na pia kuzilinganua. Wanaisimu huchunguza lugha katika viwango vyote yaani fonolojia, mofolojia, sintaksianasemantiki ili kuonyeshana kueleza jinsi lugha hizo zinavyofananapia kutofautiana. Anaendelea kusema kuwa isimu linganishi husaidia kubainisha makundi mbali mbali ya lugha. Wakati mwengine wanaisimu wanapozilinganisha lugha mbali mbali hufanikiwa kuunda lugha mame, ya lugha hizo. Kutokana na hiyo lugha mame, wanaisimu hubainisha lugha hizo na uhusiano wa kinasaba na kuonyesha jinsi lugha hizo zinavyotofautiana.

Matinde (2012), akiieleza kuhusu kiunzi hiki cha nadharia anafafanua kuwa isimu linganishi huchunguza mfanano na muachano wa lugha mbili au zaidi. Ni kutokana

tawi hili ambapo lugha mbali mbali huwekwa katika makundi kwa kutegemea uhusiano wa lugha hizo. Kwa mfano, kundi la Kibantu hujumuisha Kiswahili, Kikuria, Kisukuma, Kihaya, Kixhosa, Kikamba, Kibangada, Kiluhya nakadhalika. Matinde (keshatajwa) anendelea kueleza kuwa mwaka 1976, William Jones, msomi wa Uingereza alidai kuwa lugha ya Kisankrit, Kigiriki na Kilatini zinahusiana na kwamba zimetokana na lugha mame moja. Madai yake yalikitwa katika ufanano aliwouwona katika sauti na maana katika lugha hizo tatu.

Mnamo mwaka 1972 nadharia hii ya Isimu linganishi ilitumiwa na Raimo Anttila kulinganisha lugha za Kiswidi, Kiingereza na Kijerumani. Anttila, (1972:229) anafafanua:

... ni mbinu kuu ya isimu linganishi inayo tumiwa kuchambua lugha zaidi ya moja ambazo zina asili moja kwa lengo la kuanzisha uhusiano wao wa kihistoria (TY).

Nadharia ya isimu linganishi ina vigezo vitatu ambavyo hutumika katika kulinganisha lugha. Kigezo cha msamiati wa msingi unaohusu vitu vya kawaida katika mazingira ya wasemaji wa lugha zinazohusika, vitu vya asili katika mazingira hayo, majina ya viungo vya muili na shughuli za kila siku za jimii huska, Anasema kigezo cha pili ni kukubaliana kwa sauti katika maneno, hutumika kulinganisha sauti za maneno ya msingi ili kubaini kwa kiasigani sauti hizo zinafanana au zinatofautiana. Kigezo cha tatu ni kile cha kuchunguza ili kuona kuwa lugha hizo zina misamiati yenye maana moja yenye sauti tofauti. Maneno ambayo yanatofautiana kimaumbo lakini yanakubaliana kisauti hujulikana kama maneno mnasaba (Massamba, 2002).

Nadharia hii ya Isimu linganishi itatusaidia katika kulinganisha na kutofautisha athari za kifonolojia katika msamiati wa Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu ili kubaini tofauti za kiisimu za maneno hayo.

2.5 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii pia tumezungumzia vipengele mbalimbali vinyoyojihusisha na mada ya uchunguzi huu vikiwemo mapitio ya kazi tangulizi ambapo wataalamu mbali mbali wameangalia kuhusu lahaja za Kiswahili.vile vile tukaangalia tafiti mbali mbali zilizowahi kufanyika kwa kuangalia tofauti za kiisimu katika lahaja ya Kipemba na lahaja nyingine. Pia kuna tofauti ya wazungumzaji katika lugha moja.Kipengele chengine kilichojadiliwa ni mkabala wa kinadharia ambao umejadili kiunzi cha nadharia itakayotumika katika utafiti huu ikiwa ni nadharia ya Isimu Linganishi.

SURA YA TATU

MBINU NA NJIA ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Katika sura hii inashughulika na mbinu mbali mbali zilizotumika katika mchakato wa kufanya utafiti ili kumwezesha mtafiti kupata taarifa kwa urahisi za kuchunguza tofauti za msamati kati ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu. Mbinu hizo ni: **Ushuhudiaji, usaili, mbinu ya dodoso na mbinu ya maktaba.** Pia sura hii imegawanywa katika vipengele saba. Kipengele cha kwanza kimejadili muundo wa utafiti, kipengele cha pili kimejadili eneo la utafiti pamoja na sababu za kuteuwa eneo hilo. Kipengele cha tatu kimejadili usampulishaji kwa kuangalia aina za walengwa waliotafitiwa. Kipengele cha nne kinajadili jinsi mtafiti atakavyopata sampuli. Kipengele cha tano kimejadili mbinu mbali mbali ambazo zimetumika katika kukusanya data. Kipengele cha sita kimejadili maadili ya utafiti kwa kuangalia haki za mtafitiwa. Kipengele cha saba kinaeleza kwa ufupi jinsi data zilivyokusanywa na kuchambuliwa na mtafiti.


3.2 Muundo wa Utafiti

Cohen na wenzake (2007) wanaeleza kuwa muundo wa utafiti ni kupanga, kutoa sababu na kuzieleza data kama zilivyoelezwa na walengwa wa utafiti. Data zinapangwa kutohana na maudhui au makundi yanayolingana. Utafiti huu umetumia muundo wa kimaelezo. Muundo huu ni muhimu kwani utamsaidia mtafiti kufafanua dhana zilizofungwa, na maelezo yaliyotolewa na watafitiwa pamoja na washiriki kwa ujumla yamefanuliwa kwa kina.

3.3 Eneo ya Utafiti

Utafiti huu umefanyika katika kisiwa cha Pemba. Kimsingi, Pemba ina mikoa miwili, mkoa wa Kaskazini na mkoa wa Kusini. Mkoa ambao unatumika katika utafiti huu ni mkoa wa Kaskazini-Pemba, Wilaya ya Micheweni vijiji ambavyo vipo katika Wilaya ya Micheweni kama vile Maziwang'ombe, Kiuyu mbuyuni, Shumba – mjini, na Micheweni Chamboni. Sababu za uteuzi wa maeneo hayo ni kutokana na uzoefu alionao mtafiti na wepesi wa mtafiti wa kuchagua maeneo yanayofaa kulingana na mada na kumwezesha kupata taarifa kwa urahisina zilizo sahihi zitakazokidhi mahitaji yake

MKOA WA KASKAZINI PEMBA WILAYA YA MICHEWENI



Kielezo cha 3.1: Ramani ya eneo la utafiti:

Chanzo: <https://sw.wikipedia.org/wiki/Micheweni>. Imepakuliwa tarehe 13.01.2018

3.4 Walengwa wa Utafiti

Kundi lengwa kwa mujibu wa Cooper (1989) na Vans (1990) ni wanachama wote au hata mtu mmoja, kundi au elementi ambazo mtafiti amekusudia kuzihusisha katika utafiti wake. Utafiti umetusaida husisha watu waliozaliwa katika vijiji mbali mbali vya Micheweni ambao wameishi kwa muda mrefu na wenye umri kuanzia miaka 45 na kuendelea. Utafiti huu utatumia walengwa hao kwa sababu kundi hili halina athari kubwa ya Kiswahili sanifu na lugha za kigeni.

3.5 Usampulishaji

Sampuli ni istilahi inayotumika kumaainisha watu walioteuliwa kujibu maswala ya tafiti kutka katika kundi husika (Kothari, 1990). Katika utafiti huo sio rahisi kwa mtafiti kuwahoji wazungumzaji wote wanao zungumza Kiswahili cha Micheweni, Mtafiti atafanya utenzi wa Sampuli ilikupata kundi dogo la watu litakalowakilisha kundi kubwa.

Uteuzi wa Sampuli iliyotumika katika utafiti huu ni Sampuli tegemea-fursa (Probability Sampling) ambao umeamsaidia mtafiti kupata watafitiwa anaowataka kwa kuzingatia uwaklishaji wa kila kundi. Tulichaguwa watafitiwa kwa kuzingatia vigenzo vya umri na ukaazi. Mfano watoa taarifa ni wale watu wazima wenye umri wa miaka 45-70, wazawa wa eneo husika ambao wamekwisha kaa kwa muda mrefu katika maeneo ya Micheweni. Hii ni kwa sababu watu wazima katika maeneo hayo bado hawajaathirika na Kiswahili sanifu lakini pia hawajapata athari ya maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hivyo kumpatia mtafiti data za uhakika na kwa urahisi zaidi.

3.6 Mbinu za Kukusanya Data

Kothari (2004) anaeleza kuwa data za msingi ni zile ambazo hukusanya kwa mara ya kwanza. Data hizi zilikusanya wakati mtafiti yuko uwandani katika sehemu zilizoteuliwa. Data hizi pia zimejibu maswali ya utafiti. Data hizi zimenukuliwa kwenye madaftari na kinasa sauti. Pia kitatumika kwa ajili ya kurikodi taarifa.

Ama data za upili nizile ambazo tayari zilishakusanya na zimeshatumika na kuhifadhiwa (Kothari amekwishatajwa). Data hizi pia mtafiti alizipata kupitia maandiko ya wataalamu mbali mbali pamoja na ripoti za aina tofauti. Taarifa hizi pia zilikusanya kwa kuangalia vitabu, majorida, na machapisho mbali mbali katika maktaba kuu Pemba.

Katika utafiti huu mbinu mbali mbali za ukusanyaji data zimetumika. Kwa mujibu wa (Kothari 1990), dhana ya ukusanyaji wa data ni kama zoezi la awali katika utafiti ambalo humuwezesha mtafiti kupata tarifa alizo kusudia ili kumfikisha kwenye malengo yake ya utafiti. Kwa kuwa mbinu moja haitoshi kuhusu taarifa zinazo hitajika, utafiti huu utatumia mbinu zaidi ya moja kama vile, **Ushuhudiaji, Usaili, Dodoso, na maktaba.**

3.6.1 Mbinu ya Usaili

Mbinu hii inatumika kwa kuwasilisha maswali kwa watafitiwa, maswali ambayo yatajibiwa kwa njia ya mdomo wakati mtafiti na mtafitiwa wakiwa pamoja na hatimaye mtafiti atarekodi majibu hayo katika daftari la kumbukumbu na katika tepurekoda. Kothari (1990) anaendelea kusema mbinu hii kuwa inaruhusu unyumbukaji katika mchakto wa kuuliza maswali, na inamsaidia mtafiti kuweka

bayana istilahi ambazo hazieleweki kwa mtafitiwa. Pia mbinu hii inasaidia kupata taarifa za ziada na kwa kina zaidi kutoka kwa wanaosiliwa. Vile vile, mbinu hii inamruhusu mtafiti kuuliza maswali ya ziada na inapelekea kujenga uhusiano wa karibu kati ya mtifiti na mtafitiwa. Ingawa mbinu hii inafaida nyingi zitakazo msaidia mtafiti kupata taarifa lakini ina baadhi ya kasoro kama vile: Inapoteza muda kama ambavyo mtafiti imemsaidia mtafitiwa kutafiti mtu mmoja mmoja pamoja na kuandika au kurikodi kile ambacho kiliwasilishwa na mtafitiwa. Katika mbinu hii mtafiti amepata taarifa zinazo husiana na tofauti ya matamshi ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu.

3.6.2 Mbinu ya Dodoso

Kwa mujibu wa Kothari (keshatajwa) mbinu ya dodoso ni mbinu ya utafiti ambayo mtafiti anaandika maswali yake yanayolenga kupata taarifa kuhusu jambo fulani. Maswali haya yanaweza kuhitaji majibu mafupi au marefu kutegemea na taarifa anayoihitaji mtafiti. Mbinu hii ilitumiwa na mtafiti ili imsaidie kukusanya data ambazo mtafiti atazipata kutoka kwa wamilisi wa lugha wa eneo husika. Kukusanya data za msamiati wa Kiswahili cha Micheweni katika vijiji teule. Kwa kutumia mbinu hii mtafiti atawapa dodoso watafitiwa la orodha ya maneno na kuwataka waandike vibadala vyake kulingana na yanavyotumiwa na watumiaji wa eneo husika.

3.6.3 Mbinu ya Maktaba

Mbinu hii inahusisha mapitio ya kazi mbali mbali zilizofanywa na watafiti waliotangulia kuhusiana na mada ya utafiti. Kazi hizo zinaweza kuhusu nadharia mbalimbali au hata uchambuzi wa dhana zinazohusiana na mada ya utafiti husika kwa namna moja ama nyingine (Kothari, 1990). Katika utafiti huu mbinu hii

iliyotumika kuchunguza msamiati wa Kiswahili sanifu unavyotofautiana naKiswahili cha Micheweni. Mtafiti atapitia mbinu au sababu mbali mbali zinazochangia kuwepo kwa tofauti hizo.

3.6.4 Mbinu ya Ushuhudiaji

Kwa mujibu wa Mulokozi (1983) anaeleza kuwa mbinu ya kushuhudia ni mbinu ya kuangalia tukio linapotendeka na kukusanya taarifa zake. Mbinu hii inahitaji mtafiti kutazama wahusika wanaopendelea kuzungumza katika muktadha fulani huku akinakili mambo muhimu anayoyaona na kuyasikia (Mathooko, keshatajwa). Katika mbinu hii imemfanya mtafiti kuweza kushuhudia watafitiwa wakati wa kuzungumza na mtafiti alinakili data muhimu katika maeneo ambamo ameyafanyia kazi.

3.7 Vifaa vya Utafiti

Ili kuikamilisha kazi hii ya utafiti vifaa mbali mbali vilitumika kumsaidia mtafiti kupata taarifa sahihi na kuweka kumbukumbu za utafiti. Vifaa vilivyotumika ni pamoja na jalada, kalamu na karatasi kwa ajili ya kuandikia taarifa za watafitiwa (kuweka kumbukumbu za maeleo ya watafitiwa), simu ya mkononi kwa ajili ya mawasiliano, vinasa sauti kwa ajili ya kurikodi maeleo na sauti za watafitiwa, kompyuta mpakato kwa ajili ya kuandika pendekazo la utafiti, tasnifu na taarifa nyingine za utafiti, modemu kwa ajili ya kupakua na kuhifadhi taarifa mbali mbali zinazohusiana na utafiti.

3.8 Mbinu ya Uchambuzi wa Data

Taarifa zilizozokusanywa katika utafiti huu zimechambuliwa na kuwasilishwa kwa njia ya maeleo na majedwali kwa uchambuzi wa kimahesabu. Data ambazo

zimewasilishwa kwa njia ya majedwali pia zimefafanuliwa kwa kina kuwekewa maelezo. Mhakiki ametumia mbinu ya uchambuzi wa maelezo na vipengele vingine katika uchambuzi wa data wakati wa kufafanua tofauti za kiisimu zinazojitokeza katika utafiti huu.

3.9 Muhtasari wa Sura

Katika sura hii tumeeleza mbinu mbali mbali zitakazotumika katika mchakato wa kufanya utafiti, mbinu hizo ni kama vile mbinu ya usaili, dodoso, na maktaba. Pia vipengele vya muundo wa utafiti, maeneo ya utafiti pamoja na sababu za kuteuwa eneo hilo. Pia, kuna usampulishaji kwa kuangalia aina za walengwa waliotafitiwa. Kipengele chengine cha nne kimeeleza jinsi mtarafiti ambavyo amepata sampuli. Hata hivyo, mbinu mbali mbali ambazo ametumia mtarafiti katika kukusanya data zimeelezwa. Kuna maadili ya utafiti kwa kuangalia haki za mtarafitiwa tumeeleza kwa ufupi jinsi data zitakavyokusanywa na zitakavyochambuliwa na mtarafiti.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI WA DATA MATOKEO NA MAJADILIANO

4.0 Utangulizi

Sura hii inawasilisha matokeo yaliyopatikana kutokana na utafiti wa uwandani na utafiti wa maktabani na kuyajadili matokeo hayo. Uwasilishaji wa matokeo ulifanyika kwa kutumia Kiunzi cha Nadharia. Nadharia iliyotumika ni Isimu Linganishi. Uwasilishaji na majadiliano juu ya matokeo hayo umelenga kujibu maswali ya utafiti wa tasnifu hii katika kukamilisha malengo ya utafiti. Aidha, sehemu hii inawasilisha matokeo na kuyajadili kwa mujibu wa data iliyochambuliwa na hoja mbalimbali za wanavyuoni kama zilivyo kwenye mapitio ya kazi tangulizi katika tasnifu hii. Sura hii imegawanyika katika Sehemu vikuu vitatu. Sehemu ya kwanza imewasilisha matokeo na kuyajadili kwa kubainisha misamiati ya lahaja ya Kipemba cha Micheweni. Sehemu ya pili inawasilisha na kujadili matokeo ya misamiati ya lugha ya Kiswahili sanifu. Sehemu ta tatu itawasilisha na kujadili matokeo juu ya athari za kimawasiliano zitokanazo na tofauti za kimsamiati baina ya wazungumzaji wa Kiswahili sanifu na wale wanaozungumza Kiswahili cha Micheweni. Uwasilishaji na majadiliano ya matokeo umehusisha malengo mahsusini na kujibu maswali ya utafiti huu, baada ya kuwasilisha matokeo ya utafiti katika kila kipengele kwa kuhusisha na nadharia mbalimbali za kiisimu pamoja na hoja za wanavyuoni mbalimbali katika mapitio ya kazi zilizopita na hali halisi ya maisha ya kila siku.

4.1 Data iliyokusanywa

Data iliyokusanywa inaeleza tofauti za msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu na imegawanywa katika vipengele vya msamiati unaohusu shughuli za kilimo na ule unaohusu mazingira ya nyumbani ili kuweza kubainisha athari za kimawasiliano zinazojitokeza katika mawasiliano ya makundi hayo mawili.

4.1.1 Tofauti katika Shughuli za Kilimo

Katika Ki-Micheweni tunaona kwamba wasemaji wa maeneo hayo wanatofautiana kimatamshi na wale ambao wanazungumza Ki-Sanifu. Tofauti hiyo inaonekana kimatamshi na kimaumbo kwa baadhi ya maneno ambayo tutayaweka hapa. Uhusiano uliopo ni kuwa maana ya msamiati huo unakuwa ni sawa kama ambavyo shuguli mbali mbali za kilimo zinatendeka katika jamii zetu ispokuwa kutokana na umbali wa jiografia umefanya kuwepo kwa tofauti za matashi. Tuchunguze mifano iliyopo hapo chini:

Jedwali la 4 1:Tofauti ya Msamiati Katika Shughuli za Kilimo

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kukakata	Kulima jembe la kwanza
Ugne	Kamba
Tumbi	Pakacha
Kituwa	Mwitu/kichaka
Kuuwatiza	Kutoa mche sehemu moja na kupanda sehemu nyingine
Kuumbikia	Kupanda kabla ya mvua
Kijingwi	Kijembe kidogo cha mkono

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kukatia	Kuunganisha madongo
Guwa	Sehemu iliyolimwa ikaachwa
Chale	Sehemu iliyolimwa
Chanjaa	Sehemu isiyolimwa
Kutema	Kukata msitu
Boko	Bokoboko
Pukusi	Pukusa
Nngwe	Sehemu utakayolima
Nndu	Panga
Mboga ya viazi	Mtoriro/ mriba
Mrashi	Mchaichai
Mishonga	Majimbi
Duta	Mwinuko
Kichuguu	Kilima

Chanzo: Data ya Uwandani 2016

Katika sehemu hii ya msamiati ilichunguza msamiati unaohusiana na shughuli mbali mbali za kilimo na kuonesha tofauti iliyopo baina ya wazungumzaji wa Ki-Micheweni na Ki-Sanifu, ikiwa ni moja kati ya malengo mahsusini ya utafiti huu. Watafitiwa walishiriki ni 20 na ambao 10 walijibu maswali ya dodoso na 10 walijibu maswali ya usaili na matokeo yaliyopatikana yalithibitisha kwamba kuna tofauti kubwa ya msamiati katika shughuli za kilimo baina ya KI-Micheweni na KI-Sanifu. Maswali ya utafiti yaliwataka watafitiwa wataje vibadala vya maneno ya KI-Sanifu

katika msamiati wa KI-Micheweni na ndivyo hivyo hivyo majibu yalitolewa kwa njia ya dodosa na wengine usaili. Msamiati *duta* ambao unatumika katika Ki-Micheweni una maana ya mwinuko katika Ki-Sanifu. Tukichunguza orodha hii ya msamiati tunaweza kusema kwamba hata baadhi ya wanaisimu wamelibaini hilo na kuonesha kwamba kuna tofauti za msamiati zinazojitokeza kwa wazungumzaji. Tofauti hizo zinaweza kuwa zinatokana na maeneo wanamoishi kushindwa kuwaelewa wengine. Polome (1967) aliunga mkono dai hili alipobainisha kuwa Micheweni wanazungumza lahaja ndogo ambayo kwa kiasi fulani inatofautiana na maeneo mengine. Mfano katika *neno duta* ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *mwinuko*. Vile vile msamiatipwaza katika Ki-Micheweni una maana *chemsha* katika Ki-Sanifu.

Mifano mingine iliweza kuonekana ikioneshaa tofauti iliyodhahirishwa na wakaazi wa kijiji cha Chamboni wakati wa jioni nikiwa namsubiri mtafitiwa amalizie kupika. Nikiwa katika utafiti mara mama mzazi alimtumwa mwanawe kwa kumwambia *kageye izi ndaza* ambapo katika KI-Sanifu maneno haya yana maana *katupe hizi chichi*. Hapo hapo tukiwa katika dodoso akapita kuku akanya alichokifanya mama ni kumwambia mtoto alikuwa yumo ndani mpa ikyo kijingwi nzolele uwu uharnaneno haya katika KI-Sanifu yakiwa na maana nipa hicho kijembe nizoleye hayo mavi ya kuku.

4. 1.2 Tofauti katika mboga na Dawa za Majani

Pia kuna tofauti nyingine ya matamshi baina ya Ki-Micheweni na K-Sanifu ambazo zinatokana na kilimo cha mboga pamoja na dawa za watoto za majani. Tofauti hizo zinaoneka zikijitokeza kwa baadhi ya maneno ambayo yanatumika na wasemaji wa

viswahili hivi viwili ili kuweza kubainisha athari za kimawasiliano kupitia wazungumzaji wa maeneo hayo. Tangalie orodha ya maneno yafuatayo:

Jedwali La 4.2: Tofauti Zitokanazo na Mboga na Majani na Dawa za Watoto za Majani

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU.
Kivumbasi	Kivumbani
Muingajini	Mpambawake
Nkundenyika	Mkunde
Mboga ya viazi	Mtoriro
Kikwayakwaya	Mribaziwa

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Katika orodha ya msamiati uliopo hapo juu inaonesha kwamba kuna tofauti za matamshi baina ya wasemaji wa Ki- Micheweni na wasemaji wa Ki-Sanifu. Tofauti hiyo inaonekana kujitokeza katika baadhi ya msamiati kama vile, muingajini ni msamiati unaotamkwa na wasemaji wa Ki-micheweni lakini msamiati huo unapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka mpambawake. Vile vile, katika msamiati kikwayakwaya ni msamiati unaotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni lakini msamiati huo unapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka mribaziwa. Tofauti hizo tunazoziona hapo zinaonekana ni katika matamshi pamoja na maumbo ya maneno ilhali maana ya maneno hayo yanakuwa ni sawa.

4.1.3 Tofauti katika Mazao

Katika Ki-Micheweni tunaona kwamba kuna tofauti za kimatamshi na wasemaji wa Ki-Sanifu kupitia baadhi ya mazao ambayo wanalima wakiwa katika vilimo vyao .tofauti hizo zinaweza kubainisha katika jewdali lifuatalo:

Jedwali La 4.3: Tofauti Katika Mazao

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Tango	Boga
Hoho	Pilipili hoho
Mishonga	Majimbi
Machekwa ya kizungu	Mastafeli

Chanzo: Data za uwandani 2016

Data iliyopo hapo inabainisha tofauti za msamiatiunaohusiana na mazao yanayotumiwa na Wasemaji wa Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Tofauti hiyo imedhihirisha kuwa maneno kama vile *machekwa ya kizungu* ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutamkwa *stafeli* linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu. Vile vile neno *hoho* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *pilipili hoho* maneno yote hayo yakiwa na maana sawa katika viswahili hivi viwili.

4.2 Msamiati wa Nyumbani

Msamiati wa nyumbani umejumuisha maeneo mbali mbali ambamo hutumiwa na watumiaji wa lugha yanayowakilisha maeneo, vifaa, vyakula, pamoja na baadhi ya aina za maneno kama ambavyo ufanuzi unatubainishia. Lengo hasa ni kuonesha

tofauti za matamshi baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.tuangalie tofauti hizo kupidia vipengele vifuatavyo:

4.2.1 Tofauti ya Msamiati Unaotumika katika Mazingira ya Nyumbani

Katika sehemu hii tuliangalia msamiati wa nyumbani ikiwa ni jumla ya orodha ya maneno yanayotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni kupidia maeneo tofauti ambayo hutofautiana kimatamshi na yale ya Ki-Sanifu kama vile vifaa vinavyotumiwa na wasemaji wa Kimicheweni, maneno wanayotumia,maradhi, vyakula na mengine mengi ambayo yanapatikana katika maeneo ya nyumbani.

4.2.2 Tofauti zinazotokana na vifaa

Baadhi ya maneno yanayotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni yanatofautiana na yale ya Ki-Sanifu. Maneno hayo ni yale yanayotokanana na vifaa vyta matumizi ya nyumbani. Tunaona kwamba wasemaji wa Ki-Micheweni hutofautiana kimatamshi katika maneno yenye maana ile ile iliyoko katika Ki-Sanifu. Tuchunguze tofauti hizo katika mifano ifuatayo:

Jedwali La 4.4: Tofauti Zinazotokana na Vifaa

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Peku	Ungo mbovu
Senti	Sinia
Nkanshi	Kijiko cha mchuzi
Nchamo	Nkeka mbovu
Shana	Shanua
Dishi	Sufuria
Kibia	Chungu
Kibati	Kibakuli
Ifya	Jifya.

Chanzo: data za uwandani 2016

Kupitia mifano hiyo tunaona kwamba kuna tofauti nyingine ambayo ni ya majina ya vifaa ambavyo hutumika katika matumizi ya nyumbani jambo ambalo linakosekana kwa wasemaji wa Ki-Sanifu. Mfano neno senti ni neno ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni, neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu neno hilo hulitamka sinia. Vile vile nenou *nkanshi* ni neno ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni lakini neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hubadilika na kutamkwa kijiko. Tukiendelea mbele kuna neno *kibati* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hubadilika neno hilo na kutamkwa *kibakuli* na wasemaji wa Ki-Sanifu. Hivyo basi mifano ya maneno hayo ambayo ni ya vifaa vya nyumbani yanatofautiana ki-utamkaji kwa wasemaji wa Ki-Sanifu na wasemaji wa Ki-Micheweni lakini maneno hayo yana maana sawa katika pande zote mbili.

4.2.3 Tofauti zinazojitokeza katika Maeneo

Maeneo ni zile sehemu ambazo wanajimii wanakaa. Maeneo hayo yanatofautiana kitamkaji na waemaji wa Ki-Micheweni na waKi-Sanifu. Tuangalie mifano ifuatayo:

Jedwali La 4. 5: Tofauti zinazojitokeza katika maeneo

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Ubungu	Uwanja
Upenuni	Pembezoni mwa nymba
Kati	Chumbani
Bandani	Ukumbini
Kyuo	Chuo
Kyumba	Chumba

Chanzo: Data za uwandani 2016

Tofauti nyingine ambayo hujitokeza baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu ni katika maeneo ambayo yanapatikana katika mazungira ya nyumbani. Wasemaji ambao ni wa Ki-Micheweni hutofatiana maneno hayo kuitia maumbo na matamshi ya maneno hayo jambo ambalo haliathiri maana kwa wasemaji wa Ki-Sanifu. Kwa mfano neno *kati* ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka *chumbani*. Vile vile katika neno *ubungu* ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *uwanja*. Maneno hayo na mengine ambayo hatujayaweka hapo yanaonesha kuwa maumbo ya maneno yamesababisha kuwepo tofauti za matamshi baina ya Viswahili hivi lakini maana haikuathiriwa katika maneno hayo.

4.2.4 Tofauti zinazotokana na nomino za maradhi

Katika mazingira yetu ya nyumbani baadhi ya maradhi yanatofautiana kimatamshi kati ya Ki-sanifu Ki-Micheweni. Tofauti hiyo inawza kuwa ya ubadilikaji wa neno au sehemu katika neno hilo. Tofauti hiyo tunaweza kuithibitisha kupitia mifano ifuatayo:

Jedwali La 4. 6: Tofauti za Misamiati Kuhusu Maradhi

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kiwete	Mlemavu
Kekefu	Kwikwi
Pumbu	Busha
Nyonga	Maradhi ya mgongo
Ipu	Jipu
Kipisi	Kiungulia
Kamasi	Mafua
Taka	Usaha
Pele	Upеле

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Mifano iliyopo hapo inathibitisha kwamba baadhi ya maneno yanayotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni yanayotokana na maradhi hutofautiana kimatamshi na wasemaji wa Ki-Sanifu. Mfano neno *kekefu* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutamkwa hivyo lakini neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *kwikwi* likiwa na maana sawa na *kekefu*. Vile vile wasemaji wa Ki-

Micheweni hutamka *kiwete* na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka neno *mlemavu* likiwa na maana sawa na *kiwete*. Katika maneno hayo tunaona kwamba yanatofautiana kimatamshi na kwa upande wa maana yanakuwa ni sawa kwa viswahili vyote viwili.

4.2.5 Tofauti katika Vitenzi vyta kawaida

Vitenzi vyta Ki-Micheweni ambavyo vinatumika katika mazingira ya nyumbani vinaweza kuwa vitenzi vyta kawaida. Vitenzi hivyo vinatofautiana na vile vyta Ki-Sanifu wakati wa kutamka, kwamba wazungumzaji wa KI-Sanifu na KI-Micheweni wanatofautiana katika utamkaji wa vitenzi hivyo. Tuangalie mfano wa vitenzi vyta kawaida vinavyotumika katika mangira ya nyumbani kwenye jedwali lifuatalo:

Jedwali La 4.7: Tofauti katika Vitenzi vyta Kawaida

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kauku	Kaondoka
Tongoa	Sema/ zungumza
Kulya	Kula
Sebu	Sitaki
Keleshi	Kaakitako
Chama	Hama
Dumua	Kata
Kucha	Kuogopa
Alisa	Uguza
Dengua	Popoa

Songa	Suka
Kwama	Fukuza
Geleka	Potea
Pisa	Unguza
Penjewa	Furahi
Chunza	Angalia / tazama.
Kuuya	Kurudi
Kufisa	Kupeleka
Bofya	Bonyeza
Bauwa	Kojoa
Avya	Toa
Enza	Fuata
Twaa	Chukua
Sindika nlyango	Funga mlanga
Komoa kufuli	Fungua fukuli
Kwaga	Kupotea
Uwata	Kanyaga
Utama	Chutama
Huviji	Hujui
Pusa	Haraka
Geya	Tupa
Bwaga	Angusha
Kovyoka	Tapika

Katika orodha ya maneno yaliyopo hapo juu inaonesha kwamba kuna tofauti kubwa inyojitekeza baina ya msamiati wa Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Tofauti hizo zinaonekana kupitia vitenzi mbali mbali vinavyotumika katika mazingira ya nyumbani. Mfano msamiati keleshi unatoka katika Ki-Micheweni una maana kaakitako katika Ki-Sanifu, msamiati mwengine ni utama katika Ki-Micheweni msamiati huu una maana ya chuchumaa katika Ki-Sanifu. Pia msamiati Pisa katika Ki-Micheweni una maana ya unguza katika Ki-Sanifu. Kwa hali hii ni wazi kwamba vitenzi vya Ki-Micheweni vinavyotumika katika mazingira ya nyumbani vinatofautiana kimatamshi na vile vya Ki-Sanifu ingawa vyote vina maana yanayofanana.

4.2.6 Tofauti Katika Viulizi

Katika viulizi kuna tofauti kubwa kwa wazungumzaji ambao si waMicheweni kutofahamu kile ambacho kinazungumzwa, hali hii ni kuonesha kwamba wazungumzaji hawa hawatumii Ki-Sanifu katika mazungumzo yao. Ithibati hii inaonekana kwa baadhi ya vitenzi viulizi vinavyobeba nafsi na vile vya kuonesha.

Jedwali la 4.8: Tofauti katika Viulizi

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Ani?	Nani
Vii?	Vipi?
Waa?	Wapi?
Kii?	Kipi?
Nii?	Nini?
Ngaa?	Ngapi?

Chanzo: Data ya Uwandani (2016)

Msamiati uliopo hapo unawakilisha baadhi ya viulizi ambavyo vinaonesha tofauti kati ya Ki-Sanifu na Ki-Micheweni. Tofauti inaonesha kwamba katika orodha ya maneno hayo kama vile Vii?, waa?, kii?, nii?, ani?, ngaa? Yanatumika katika mazingira ya kawaida ya nyumbani. Mfano, yuvii, yuwaa?, nkii?, wa ani? Pesa ngaa? mwana wa ani?, msamiati huo huo unapotumika katika Ki-Sanifu unakuwa yuko vipi?, yuko wapi?, ni kipi?, wa nani?, shilingi ngapi?. Wazungumzaji wa Ki-Micheweni katika utamkaji wa maneno hayo wanaacha baadhi ya herufi tu lakini dhana inayowakilishwa inakuwa ni sawa na ile ya Ki-Sanifu. Hivyo basi ni jambo ambalo limefanya matamshi ya pande hizo mbili kuweza kutofautiana.

Jedwali La 4.9: Tofauti Katika Vivumishi

Jedwali no 11 Tofauti katika vivumishi vya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kyangu	Changu
Kidigi	Kidogo
Kimbamba	Chembamba
Hino	Hilo
Kyepeu	Chepesi
Kyema	Kizuri
Kyadanda	Chang'ara

Chanzo: Data ya uwandani 2016

Jedwali liliopo hapo linaonesha msamiati unaotuka katika mazingira ya nyumani ambao ni wa Ki-Micheweni ukitofautana na Ki-Sanifu. Tofauti ni ya upande wa

vivumishi tu, ingawa maana zote ni sawa lakini matamshi ni tofauti. Mifano mingine ni kama vile –*vye* katika Ki-Micheweni ikiwa na maana ya *vyake* katika Ki-Sanifu, katika neno *hebuvye*. Vile vile, ikyo katika Ki-Micheweni lina maana ya hicho katika Ki-Sanifu. Hivyo hivyo na orodha iliyopo hapo inatofautisha kwamba vivumishi hivi vinatofautiana kimatamshi. Tofauti hii inapelekea wale ambao hawaishi katika mazingira hayo kutofahamu baadhi ya maneno yamekusudiwa nini au yana maana gani. Hivyo ni tofauti ambazo zinalenga moja kwa moja na kunesha matamshi ya Kimicheweni yanatofautiana na Kisanifu kwa kuwa wanamicheweni bado Kiswahili chao hakijaathiriwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia.

4.2.7 Tofauti Katika Nomino

Katika mazingira ya Micheweni baadhi ya nomino zinatofautiana kimatamshi na zile ambazo zinatzmkwa katika Ki-Sanifu. Hali hii inaonekana kwamba hadi sasa Wanamicheweni hawajapata mabadiliko ya hali ya juu ambayo yanaweza kubadilisha vitu wanavyotumia, vilivyowazunguka au hata vile wanavyotengeneza wao wenyewe, kama vile vitu vinavyotumika katika mazingira ya nyumbani vyta matumizi ya jikoni, ndani ya nyumba au hata nje ya nyumba. Majina hayo yanaweza kuwa ni yale yenyе asili ya kibantu au yanayotoka katika lugha za kigeni. Tukiangalia yote hayo kimatamshi yanatofautiana na yale ambayo ni ya Kisanifu. Jadweli liliopo hapo linathibitisha hayo.

Jedwali La 4.10: Tofauti Katika Nomino za Ki-Micheweni na Ki-Sanifu Yenye

Asili ya Kibantu

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kyombo	Chombo
Kibati	Kibakuli
Kinyaa	Uchafu
Kibia	Mkungu
Buli	Birika
Ndaza	Chicha
Kijio	Chajio
Vishuka	Chamchana

Chanzo: Data ya uwandani 2016

Msamiati tuliuonesha hapo unaonesha kwamba ni msamiati wenyе asili ya Kibantu ambao unatumika katika Ki-Micheweni unaotofautiana na ule wa Ki-sanifu. Hali hii tumeweza kuiona kupitia mifano mbalimbali ya msamiati ambapo tunaona katika Ki-sanifu neno kama *chamchana* linatumika *vishuka* katika Ki-Micheweni. Vile vile katika Ki-Sanifu neno *chichi* linatumika *ndaza* katika Ki-Micheweni. Hata orodha ya maneno yaliyopo hapo yanatoa uthibitisho kuwa Ki-Micheweni kinatofautiana na Ki-Sanifu katika msamiati wake.

4.2.8 Tofauti Katika Nomino za Ki-Micheweni na Ki-Sanifu Zenye Asili ya Lugh za Kigeni

Hata hivyo kwa kuwa Tanzania ni mionganini mwa nchi zilizotawaliwa na eneo la Micheweni limo ndani ya Tanzania kuna baadhi ya maneno katika mazingira ya

nyumbani yalitokana na wageni walioingia na kutoka katika nchi hiyo, pamoja na maneno hayo hata wale walioingia kwa sababu zao mbalimbali walichangia kupatikana kwa msamiati. Vile vile maneno mengine ya kigeni yaliweza kuchukuliwa katika lugha za kigeni kwa ajili tu ya kuwafanya Wanajamii wakidhi mahitaji yao Kimsamiati.

Jedwali La 4.11: Tofauti za Nomino Zenye Asili ya Lugha za Kigeni

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Dishi	Sufuria
Besi	Beseni
Aridhi	Durusu
Unju	Asubuhi
Badia	Bajia
Achari	Achali

Chanzo: Data ya uwandani 2016

Msamiati uliopo hapo niuthibitisho kwamba hata yale maneno ya kigeni yanatumika katika Ki-Micheweni lakini yanatofautina kimatamshi na Ki-Sanifu ingawa yanaonesha yote yana maana sawa. Wazungumzaji wa Ki-Micheweni msamiati wanaoutumia kama vile *dishi* unatofautiana na ule wa Ki-Sanifu wenye maana sawa na *sufuria*. Vile vile neno *unju* ambalo hutumiwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotumiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *asubuhi*. Hivyo basi inaonesha hata maneno ya kigeni yanatumika na wanamicheweni matamshi yao yanatofautiana na Ki-Sanifu.

4.2.9 Tofauti za Majina ya Wadudu

Katika uchunguzi tumebaini kwamba kuna baadhi ya msamiati unaohusiana na majina ya wadudu ambao huonekana katika mazingira ya nyumbani ukitofautiana kimatamshi baina ya kimicheweni na ule naotamkwa na waseji wa kisanifu. Tofauti hiyo inaegemea zaidi katika utamkaji jambo ambalo baadhi ya maneno yanapotamkwa kwa wale ambao si wakaazi wa maeneo hayo wanashindwa kuelewa jambo gani msemaji amekusudia. Tuangalie jedwali lifuatalo:

Jedwali La 4.12: Tofauti za Majina ya Wadudu

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kurumbiza	Kurumbizi
Ndudu masika	Kumbikumbi
Nyange	Hariri
Kupa	Kupe
Kicho	Panya
Shawa	Chawa
Pepe	Mende

Chanzo: data za uwandani: 2016

Mifano iliyopo hapo inathibitisha kuwa kuna tofauti za matamshi zinazoonekana katika maumbo ya msamiati uliopo hapo katika Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Tofauti hizo zimejidhihirisha kupitia viswahili hivyo viwili katika baadhi ya wadudu tuliowaorodhesha hapo. Kama vile msamiati pepe ni msamiati unaotamkwa hivyo na wasemaji wa Ki-Micheweni lakini msamiati huo unapotamkwa na wasemaji wa Ki-

Sanifu hutamka mende. Vile vile wasemaji wa Ki-Micheweni hutamka msamiati nyange ambapo msamiati huo unapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka Hariri. Tofauti hiyo tuliyoina imedhihirisha kwamba kilifanya tofauti za matamshi baina ya viswahili hivi viwili nimaumbo ya maneno pekee ila kwa upande wa maana msamiati huo uko sawa kwa viswahili vyote viwili.

4.2.10 Tofauti ya Majina ya Ukoo

Tofauti nyingine inayojitokeza Kwa wasemaji wa Ki-Sanifu na Ki-Micheweni ni ile ya majina yenhe uhusiano wa kiukoo ambayo majina hayo yanapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutofautiana kimatamshi na wasemaji wa Ki-Sanifu.

Data ifuatayo inathibitisha hayo:

Jedwali La 4.13: Tofauti za Majina ya Ukoo

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Nkazahau	Mke wa mjomba
Wifi	Mke wa kaka
Mameye	Mamayake
Mame	Mama
Mamenkuu	Mama mkubwa
Kake	Kaka
Dade	Dada
Muamu	Shemegi
Mendogo/ mamendogo	Mamamdogo/ haloo

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Katika mifano hiyo tumeonesha tofauti za matamshi baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu zikiwemo za msamiati oamoja na maumbo ya maneno hayo. Tofauti hizo zinazojitokeza katika pande zote mbili hazijaonesha kwamba kuna tofauti ya maana ambayo inabadilika kwa maneno yenyе vibadala katika Ki-Sanifu na Ki-Micheweni, ispokuwa ni upande wa utamkaji tu wanavyotamka wasemaji wa Ki-Micheweni katika mifano ya maneno hayo kama vile *dade* wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka *dada*. Vile vile neon *mamenkuuni* neon linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni ambapo linapotamkwa neon hilo na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *mamamkubwa*. Kwa hivyo maneno hayo yanathibitisha kwamba wasemaji wa Ki-Micheweni hutofautiana kimatamshi na wasemaji wa Ki-Sanifu.

4.2.11 Tofauti za Misamiati Inayohusu Vyakula

Kwa kawaida wasemaji ambao hawaishi eneo moja huwafanya watofautiane kimatamshi kama ambavyo tofauti hii inajitokeza baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu tofauti hiyo inaonekana hata katika baadhi ya vyakula ambavyo maeneo hayo wanatumia jambo ambalo linaonesha wakaazi wa Ki-Micheweni hutamka vyakula hivyo tofauti na Ki-Sanifu ingawa matumizi pamoja na maana ya maneno yanayotumika kuwakilisha vyakula hivyo ni sawa. Tuchunguze mifano katika jedwali lifuatalo:

Jedwali La 4.14: Tofauti za Misamiati Inayohusu Vyakula

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Mwiku	Uporo
Mapota	Maziwa mabivu
Kijio	Chajio
Vishuka	Chamchana

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Jedwali liliopo hapo linatuonesha msamiati ambao ni wa Ki-Micheweni ukitofautiana na ule wa Ki-Micheweni ambao unahusiana na vyakula vinavyotumika katika pande zote mbili. Msamiati huo umethibitisha kwamba tofauti iliyopo ni ya matamshi tu ambayo haikuathiri maana ya msamiati huo, mfano msamiati kijio ambao unatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutamkwa hivyo wakati wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkachajio. Vile vile msamiati mapota ambao unatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni unapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka maziwa *mabivu/ mtindi*. Msamiati huo ni uthibitisho wa kipengele kingine ambacho kinaonesha tofauti za matamshi baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.

Katika sehemu hii tumebainisha tofauti mbali mbali za kimsamiati kwa kuyaweka maneno yenye makundi tofauti yanayotokana na mazingira ya nyumbani. Maneno hayo yameweza kubainisha tofauti mbali mbali za kimsamiati pamoja na tofauti za kimaumbo baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Katika kujumuisha tofauti hizo tuliweza kuweka msamiati unaohusiana maradhi/ magonjwa, vifaa vya matumizi ya nyumabani, maeneo yaliyo katika mazingira ya nyumbani, msamiati wa ukoo,

msamiati wa maneno ya kigeni, msamiati wa maneno yenyeye asili ya kibantu pamoja na baadhi ya aina za maneno kama vile nomino, vivumishi, vitenzi na viulizi. Sehemu hii pia imeweza kutuonesha kwamba tofauti hizo ni katika matamshi tu lakini kwa upande wa maana yanaonesha kuwa ni sawa.

4.2.12 Tofauti Zinajitokeza Katika Matamshi

Matamshi ni neno linalotokana na neno tamka ambalo lina maana ya kitendo cha kutoa nje ya kinywa au puanī mwa mwanadamu, sauti ambazo hutumika katika mazungumzo au usemajji wowote uwao (Kihore na wenzake: 2003). Kutokana na kuwa kuna tofauti ya utamkaji wa msamiati baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu zitokanazo na tofauti za kimatamshi, tofauti hizo zinajitokeza kwa baadhi ya maneno ambayo wazungumzaji wa viswahili hivi viwili ambapo katika utamkaji wa sauti fulani ambayo hutamkwa na wazungumzaji wa eneo fulani sauti hiyo hiyo hutofautiana inapotamkwa na wasemaji wa eneo jingine.

Hali hii huyafanya maneno yaye na mwonekano tofauti ingawa maneno hayo yana maana sawa au maana zinakaribiana kwa wasemaji wa viswahili vyote viwili. Tofauti hizo pia hupelekea kutokea kwa mabadiliko ya baadhi ya silabi katika maneno ambayo yanatamkwa na wasemaji wa eneo moja na jingine. Tofauti hizo zinatokana na kifonolojia ambazo ufanuzi wake hautakuwa kwa kina zaidi ila tutafafanua kwa kifupi tu kwa kubainisha mifano na namna ambavyo ilitofautiana katika Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Hata hivyo tofauti hii ya matamshi baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu hupelekea wasemaji wa Ki-Micheweni kuonesha athari za mabadiliko ya maneno mbali mbali yanayozungumzwa na wasemaji yatokanayo na fonolojia kama vile kuwepo udondoshaji wa baadhi ya sauti, kuwepo kwa

ukaakaishaji, kubadili fonimu au sauti. Hali hii inaonesha kwamba wasemaji hawa bado hadi sasa hawajaathiriwa na Kiswahili sanifu. Katika ufanuzi wa kipengele hiki tutakifafanua kupitia athari za kimawasiliano zitokanazo na fonolojia zinazosababisha kuwepo tofauti za matamshi baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu.

4.3 Athari za Kimawasiliano Zitokanazo na Tofauti za Msamiati Bainya ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu

Katika kipengele hiki tuaangalia namna gani matamshi ya Kswahili cha Micheweni nayale Ki-Sanifu yanatofautiana kupitia athari zinazotokana na fonolojia. Athari hizo tunaweza kuzibainisha kwa kuzingatia vipengele vifuatavyo. Bila kuzichambua kiundani kwani si mionganoni mwa malengo ya utafiti huu.

4.3.1 Mfumo wa Sauti

Kabla hatujabainisha nia athari gani za kimatamshi zinazokuwepo baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu hatuna budi kuangalia mfumo wa sauti zinazotumika katika Ki-Sanifu na baadae kuweza kuona katika Ki-Micheweni kwa sababu lugha pia hutofautiana kupitia idadi ya sauti zitumikazo katika lugha hiyo. Sauti hizo tunaweza **kuzianisha katika irabu, konsinanti pamoja na viyeyusho.**

4.3.2 Irabu

Ni kitamkwa ambacho hutolewa pasi na kizuizi chochote kile katika mkondo hewa utokao mapafuni kupitia chemba ya kinywa (Massamba na wenziwe, 2004). Katika Ki-Micheweni irabu zake zinalingana na zile za Ki-Sanifu kwani katika viswahili hivi viwili vyote vina irabu tano ambazo ni, **a,e,I,o,na u**, irabu hizo ingawa ni sawa

ki-idadi ila tofauti inajitokeza katika utamkaji wa baadhi ya maneno katika Ki-Micheweni. Kielelezo kifuatacho kinaonesha irabu za Kiswahili.

Kielelezo cha 4.1 :Irabu Msingi za Lugha za Ki-Sanifu

Kutokana na jadweli liliopo hapo ni wazi kuwan Ki-Micheweni kinairabu sawa na Ki-Sanifu. Irabu hizo ni **I**na **u** ni irabu za juu, **e** na **o** ni irabu za kati na irabu **a** ni irabu , irabu chini na irabu nyingine ni **I** na **e** ni irabu mbele na hutamkwa kwa mtandazo wa mdomo, na irabu o na u ni za nyuma na hutamkwa kwa midomo iliyoviringwa. Pia irabuahutamkwa kwa mdomo mtandazo. Ingawa irabu ni sawa za Kisani na Ki-Micheweni lakini tofauti inaonekana katika Kimicheweni hurefusha baadhi ya irabu katika neno na kuwa na maana 54 asana kama kwamba ni maneno mawili yaliyotumika hapo. Jambo ambalo linaonesha kwamba ni mionganii mwa tofauti zinaojitokeza katika viswahili hivi viwili. Mifano ifuatayo inathibitisha tofauti hizo zinazotakana na urefushaji wa irabu katika Ki-Micheweni ambaa urefushaji huu ni tofauti na ule unaozoeleka wa Ki-Sanifu unaoainishwa kwa kutumia nukta mbili [:]

Jedwali La 4.15. Irabu Katika Ki-Sanifu

Msamiati	Irabu iliyorefushwa	
Pekee	[ɛ:]	[peke:]
Komaa	[a:]	[koma:]
Kunguu	[u:]	[kungu:]

Chanzo: (Mgullu, 1999)

Jedwali La 4.16: Irabu Katika Ki-Micheweni

Msamiati wa Michewei	Urefushaji unaojitokeza.	Ki-sanifu
Kidiigi	[kidi:gi]	Kidogo sana
Kifuupi	[kifu:pi]	Kifupi sana
Mjeuuri	[mjeu:ri]	Mjeuri sana
Kanliaaa	[kanlia:]	Amelia sana

Chanzo: Data ya Uwandani-2016

Majadweli yaliyopo hapo yanaonesha kwamba kuna tofauti kati ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu katika urefushaji wa irabu na kuthibitisha KiMicheweni kina urefushaji ambao unachukua nafasi neno jingine lenye maana y *asana* katika Ki-Micheweni. Urefushaji huo unaweza kujitikeza katika aina mbali mbali za maneno kama vile vitenzi, vivumishi, nomino na aina nyengine za maneno. Katika vitenzi urefushaji unajitokeza kwenye silabi ya mwisho ya neno lakini pia katika vivumishi urefushaji unajitokeza kabla ya silabi ya mwisho ya neno. Hata hivyo urefushaji katika nomino unaweza kujitokeza katika silabi ya tatu ya neno.

4.3.3 Konsonanti

Konsonati ni aina ya sauti ambazo hutamkwa kwa kuzuia mkondohewa kutoka mapafuni, ukipitia chemba ya kinywa na chemba ya pua kwenda nje1. Kiswahili sanifu kina jumla ya kosonanti 23 zinazotumika katika mfumo lugha wa matamshi na maandishi. Konsonanti hizo **nib**, **ch**, **d**, **dh**, **f**, **g**, **gh**, **h**, **j**, **k**, **l**, **m** na **n**. Nyingine ni **ny**, **ng'**, **p**, **r**, **s**, **sh**, **t**, **th**, **v** na **z**. Kama tulivyobaini kwamba mifumo ya irabu katika Ki-Micheweni inalingana na mfumo wa irabu wa Kisanifu, hali ni vivyo hivyo kwa

upande wa mfumo wa konsonanti na viyeyusho baina ya Kisanifu na Ki-Micheweni inatofautiana kwa baadhi ya konsonati kwani Ki-Micheweni kina konsonanti 29 zinazotumika katika mfumo wa lugha wa matamshi. Konsonanti hizo ni **b, ch, ch, d, dh, f, g, gh, h, j, k, kh, ky, l, ly, m na n, ny, ng', p, ph, r, s, sh, t, th, th, v na z.** Kwa kweli, sauti [ky] na [ly]zinapatikana katika Ki-Micheweni tu na hazipatikani katika Ki-Sanifu.

4.3.4 Viyeyusho

Viyeyusho ni aina ya sauti ambazo haziko kwenye konsonati wala irabu kwa maana hiyo ni sauti ambazo huchukuliwa kuwa ziko baina ya irabu na konsonanti. Kiswahili kina viyeyosho viwili, ambavyo ni *w* na *y*. Tukiangalia idadi pamoja na aina za viyeyusho katika Ki-Micheweni na Ki-Sanifu ni sawa ispokuwa kuna tofauti ya matamshi kwa Ki-Micheweni. Tofauti hizo zinajitokeza katika maeneo mbali mbali kama vile:

Kielelezo cha 4. 2. Konsonanti

Aina	Midomo	Midomo	Meno	Meno	Ufizi	Kaakaa	Kaakaa	Glota	Jumla
		Na Meno		Na ufizi		gumu	laini		
1.Vikwamizwa		Fv	Өð		sz	š	kg	h	
2.Vizuio	pb				td				
3.Nasali	M				n	ñ	ŋ		
4.Vizuio Kwamiza						j č			
5.Kitambaza					I				
6.Kimadende					r				

Chanzo: Mgullu (1999)

Kwa kuzingatia sifa ya mahali pa matamshi, konsonanti za Kisanifu huweza kuainishwa katika makundi mengine saba yaani, kuna konsonanti zenyе sifa ya: *midomo, midomo meno, ufizi meno, ufizi, kaakaa gumu, kaakaa laini na koromeo.* Jedwali liliopo hopo linaonyesha sifa za kimatamshi za konsonanti na viyeyusho vya Kisanifu

4.3.5 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti

Katika Ki-Micheweni baadhi ya sauti hutofautiana na Ki-Sanifu katika utamkaji wa sauti hizo. Mara nyingi ni zile sauti ambazo zinatokana na athari za maneno ya kigeni kama vile sauti [th], [gh], [dh], [kh], nazile sauti ambazo zinatokana na maneno ya kibantu kama vile sauti [m], [n], [ch], [sh]na nyenginezo. Ama zile sautu za kigeni ni kwamba maneno ambayo mara nyingi yanatumia sauti hizo ni yale yenye athari za lugha za kigeni kama alivyosema (Massamba, 2006) kwamba ingawa sauti hizi zinatumika katika baadhi ya lugha za Kibantu na hata katika Ki-Sanifu sauti hizo zinapatikana lakini ukweli ni kwamba sauti hizo zimetokana na maneno

Yaliyokopwa kutoka lugha ya Kiarabu. Hivyo, sauti hizo katika Ki-Micheweni na Ki-Sanifu zinatofautiana kama ifuatavyo:

4.3.6 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [gh]:[h]

Watamkaji wa Ki-Micheweni wanatofautiana na wale wa Ki-Sanifu kwa sababu Ki-Micheweni hutumia sauti [h] badala ya [kh] ambayo hutamkwa katika Ki-Sanifu. Tuangalie mifano ifuatayo katika jadweli liliopo hapa chini:

Jedwali La 4.17: Tofauti za Mabadiliko ya Sauti [gh] : [h].

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Balehe	Baleghe
Hairi	Ghairi
Shuhuli	Shughuli
Kuhani	Kughani
Horofa	Ghorofa
Hafula	Ghafla

Chonzo: Data za Uwandani (2016)

Kwa maana hiyo tunaweza kusema mifano iliyopo hapo inathibitisha kwamba wasemaji Waliowengi wanaozungumza Ki-Micheweni wanatamka sauti [h] ambayo ni ya kiwamizi ghuna cha koromeo na kuacha ile ya K-Sanifu sauti [gh] ambayo ni kikwamizi ghuna cha kaakaa laini. Mfano neno horofa ni neno ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni ila neno hilo hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka ghorofa kwa sababu wasemaji hao hakuna mabadiliko ya sauti [gh] kama ambavyo inabadilika katika Ki-Micheweni. Vile vile neno *shughuli* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutamkwa *shuhuli* likiwa neno hilo lina mana sawa na lile linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu.

4.3.7 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [dh]: [z]

Vile vile utamkaji wa sauti [dh] baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu unaonekana kwani wasemaji wa Ki-Sanifu huitamka [dh] lakini wasemaji wa Ki-Micheweni huitamka sauti hiyo kama [z]. Baadhi ya mifano inayothibitisha ni kama hii ifuatayo:

Jedwali La 4.18: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [dh]: [z]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Zarau	Dharau
Feza	Fedha
Zahabu	Dhahabu
Hazira	Hadhira
Azuhuri	Adhuhuri
Hazarani	hadharani

Chanzo; Data ya uwandani (2016)

Mifano iliyopo hapo inadhihirisha kuwa katika Ki-Micheweni mahala pa sauti [dh], ambayo ni kikwamizi ghuna cha mano huwekwa sauti [z] ambayo ni kikwamizi ghuna cha ufizi, lakini kwa upande wa Ki-Sanifu hutamkwa hivyo hivyo [dh]. Maneno hayo ni kama vile azuhuri ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka adhuhuri kwa sababu ya kutobadilika sauti[dh] katika baadhi ya maneno na kuwa sauti [z] kama ambavyo inatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni.

4.3.8 Tofauti ya Mabadiliko ya Fonimu [m] kuwa [n]

Kama tulivyotangulia kusema kuwa wazungumzaji wa Ki-Micheweni hutofautiana na wazungumzajikatika Ki-Sanifu kutokana na baadhi ya sauti au finimu kwa baadhi ya wazungumzaji kuzitamka kulingana na uzungumzaji wa eneo husika. Mabadiliko haya yanajitokeza kwa kiasi kikubwa ila katika herufi [m] ambayo inatumika katika baadhi ya maneno kwa Ki-Sanifu hubadilika kuwa [n] kwa wazungumzaji wa Ki-Micheweni. Tuangalie tofauti hizo katika mifano ifuatayo:

Jedwali la 4.19: Tofauti ya Mabadiliko Fonimu [m] Kuwa [n]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Nchele	Mcchele
Nkeka	Mkekka
Nkate	Mkate
Nkoba	Mkoba
Njomba	Mjomba
Sanli	samli

Chanzo: Data ya Uwandani (2016)

Kama tulivyoangalia msamiati wenyе fonimu [m] inaposimama pekee kama silabi hutamkwa [n] kwa wasemaji wengi wa Ki-Micheweni wakati kwa wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka hivyo hivyo [m]. kwa mfano katika Ki-Micheweni hutamka neno *nkoba* kwa kuanzia na sauti [n] ya nazali midomo lakini kwa wale wa Ki-Sanifu hutamka neno hilo kwa kutumia *mkoba* kwa kuazia na sauti [m] ya nazali ufizi. Vile vile, neno *nkate* hutamkwa katika katika Ki-Micheweni wakati katika Ki-Sanifu neno hili hili hutamkwa *mkate*. Hali hii imepelekea kuonesha namna gani fonimu [m] ambayo hutamkwa katika Ki-Sanifu hubadilika na kutamkwa [n] katika Ki-Micheweni, ikiwa zote hizi ni athari zilizopelekea kutokea mkwa tofauti za msamiati baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu ingawa maana ya maneno haya yanakuwa ni sawa.

Kwa upande mwengine sauti [m] hubadilika inapoambatana na herufi [r] katika Ki-Micheweni na katika Ki-Sanifu, kwa mfano katika neno *mrefu* ambalo hutamkwa

katika Ki-Sanifu hubadilika na kutamkwa [nd] katika neno *nndefu*. Vile vile neno *mrembo* ambalo hutamkwa katika Ki-Sanifu hubadilika na kutamkwa *nndembo* katika Ki-Micheweni.

4.3.9 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [j]: [z]

Tofauti nyingine ni ile ya utamkaji wa sauti [j] baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu kwa baadhi ya maneno. Wasemaji wa Ki-Sanifu huitamka sauti hiyo kama kawaida ilivyo katika Ki-Sanifu [j] ambapo wasemaji wa Ki-Micheweni huibadilisha na kuitamka [z]. Mifano ifuatayo inadhihirisha jambo hili:-

Jedwali la 4.20: Tofauti ya Mabadiloko ya Sauti [j]Kuwa [z].

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Zicho	Jicho
Zino	Jino
Zina	Jina
Ziko	Jiko

Chanzo: Data za Uwandani (2016)

Mifano iliyopo hapo inathibitisha kuwepo kwa tofauti za utamkaji wa suti [J] na kuwa sauti [z] katika Ki-Micheweni jambo ambalo wasemaji wa Ki-Sanifu huitamka hivyo hivyo bila kuweka mabadiliko yejote. Mfano wasemaji wa Ki-Micheweni hutamka neno zino lakini neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *jino*, mfano mwengine ni *jiko* ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu , neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hulitamka neno hilo

ziko. Kielelezo kilichopo hapo kimeweka bayana tofauti za mabadiliko ya sauti [j] inapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni huitamka [z].

4.3.10 Tofauti za Mabadiliko ya Sauti [z] kuwa [v]

Tofauti nyengine ambayo hujitokeza katika utamkaji baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu ni ile ya badiliko la sauti [z] ambayo hutamkwa katika Kiswahili sanifu, sauti hiyo inapotamkwa na wazungumzaji wa Ki-Micheweni huitamka [v] kwa baadhi ya maneno. Mifano iliyopo hapo chini itoa ithibati ya tofauti hiyo.

Jedwali la 4.21: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [z] Kuwa [v]

Ki-Micheweni	Ki-Sanifu
Mwivi	Mwizi
Ngovi	Ngozi
Mjuvi	Mjuzi
Nkwevi	Mkwezi

Chanzo: Data ya Uwandani 2016

Katika mifano hiyo tunaona kuwa sauti [z], ambayo ni kwamizi ghuna cha ufizi, hutumiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu lakini sauti hiyo hubadilishwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutumia [v] badala yake. Ikiwa Sauti [v] ni kwamizi ghuna cha midomo na meno. Mfano neno *mwivi* ni neno linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni, neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *mwizi*. Hata hivyo, neno *ngovi* ni neno linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu lakini neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hulitamka *ngovi* kwa kubadili

sauti [z] ambayo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu na kuwa [v] ambayo inatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni. Hivyo hali hiyo imeweza kubainisha tofauti za ubadilishaji wa sauti [z] ambayo hutamkwa katika Ki-Sanifu na kutamkwa [v] katika Ki-Micheweni.

4.3.11 Tofauti ya mabadiliko ya sauti [ch] kuwa [sh]

Tofauti nyingine iliyoko ni ile ya sauti [ch] inayotamkwa katika Ki-Sanifu ambapo hubadilika sauti hii na kutamkwa [sh] katika Ki-Micheweni. Tofauti hizo hujitokeza pale ambapo sauti [ch] ambayo ni kizuiwa-kwamizi kisoghuna cha kaakaa gumu hutamkwa kamasauti [sh] ambayo ni kiwamizi kisoghuna cha kaa kaa gumu. Mwonekano wa tofauti hizo uajitokeza katika baadhi ya mifano ifuatayo:

Jedwali la 4.22: Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [Ch] kuwa [Sh]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Shaza	Chaza
Nshi	Nchi
Shawa	chawa
Shumvi	Chumvi
Shungwa	Chungwa
Nshekwa	Mchekwa

Chazo: Data za Uwandani 2016

Mifano iliyop hapo inaonesha kuwa katika Ki-Micheweni sauti [ch] ambayo ni ya kizuiwa-kikwamizi kisoghuna cha kaakaa gumu hutamkwa sati [sh] ambayo ni ya kiwamizwa kisoghuna cha kaakaagumu. Ikiwa msamiati huo una maana sawa .mfano

neno *shumvini* neno ambalo linatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkachumvi. Vile vile neno *nshi* ni neno linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Mcheweni, neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *nchi*. Tofauti hiyo ni ile ya mabadiliko ya sauti [ch] ambayo inatamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu na kutamka [sh] kwa wasemaji wa Ki-Micheweni.

4.3.12 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [sh] kuwa [s]

Vile vile kuna tofauti nyingine ya utamkaji wa sauti [sh] ambapo sauti hiyo hutamkwa kama ilivyo katika baadhi ya maneno katika Ki-Sanifu lakini sauti hizo zinapotamkwa katika Ki-Micheweni hutamkwa kama sauti [s]. Hali hii hupelekea kutokea kwa tofauti za matamshi kwa viswahili hivi viwili. Tuangalie mifano ifuatayo

Jedwali La 4.23: Tofauti Za Mabadiliko Ya /Sh/ - /S/

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Mpisi	Mpishi
Mosi	Moshi
Singo	Shingo
Matapisi	Matapisi

Chanzo. Data za uwandani 2016

Mifano iliyopo hapo inabainisha kuwa Ki-Sanifu kina tofautiana kimatamshi na Ki-Micheweni kutohana na mabadiliko ya sauti [sh] ambayo hutamkwa katika Ki-Sanifu, sauti hiyo inapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni huitamka sauti hiyo

kama [s]. Mfano huu unadhihirika kupitia neno *singo* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *shingo*. Vile vile mfano mwengine ni katika neno *mosi* ambalo hutamkwa katika Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa katika Ki-Sanifu hutamkwa *moshi*. Tofauti iliyojitokeza hapo ni ile ya mabadiliko ya sauti [sh] kuwa [s]. Lakini maana za maneno hayo yanakuwa ni sawa.

4.3.13 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [s] kuwa [sh]

Kwa upande mwengine kuna tofauti ya utamkaji wa maneno baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu kupitia sauti [s] ambayo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu, sauti hiyo hubadilika inapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni na huitamka sauti hiyi [sh]. Baadhi ya maneno yanayoonesha tofauti hizo ni kama vile:

Jedwali La 4. 24: Tofauti za Mabadiliko ya [S]-Kuwa [Sh]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Shindano	Sindano
Shikio	Sikio
Matushi	Matusi
Shindikiza	Sindikiza
Shurua	Surua

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Mifano iliyopo hapo inatibitisha kwamba wasemaji wa Ki-Micheweni wanatofautina kimatamshi na wale wa Ki-Sanifu kutokana na kwamba wasemaji wa Ki-Sanifu huitamka sauti hiyo kama ilivyo yaani[s] kwa baadhi ya maneno lakini kwa upande

wa Ki-Micheweni sauti hiyo hubadilika na hutamkwa [sh] jambo ambalo huathiri utamkaji wa msamiati huo. Mfano katika neno *shikio* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni, neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka *sikio*. Vile vile neno *matusi* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutamka *matushi*. Tofauti hiyo imejitokeza kupitia mabadiliko ya sauti [s] ambayo inatamkwa na waseji wa Ki-Sanifu na kuwa [sh] katika Ki-Micheweni.

4.3.14 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [th] kuwa [s]

Hata hivyo kuna tofauti nyengine ya utamkaji wa sauti [th] baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka [th] wakati wasemaji wa Ki-Micheweni hutamka sauti hiyo kama [s]. Tofauti hizo zinaonekana kupitia baadhi ya msamiati unaoonekana katika jedwali lifuatao:

Jedwali la 4.25: Tofauti Ya Sauti [Th] Kuwa [S]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Samani	Thamani
Hanisi	Hanithi
Sawabu	Thawabu
Salasini	thelathini
Hadisi	Hadithi

Chanzo: Data ya Uwandani 2016

Kutokana na mifano hiyo tunaweza kusema kuwa katika Ki-Micheweni mahali panapotamkwa sauti [th] ambayo ni kikwamizi cha kisoghuna cha meno, huwekwa

sauti [s] ambayo ni kikwamizi kisoghuna cha ufizi. Kwa maana hiyo ndiyo tukapata maneno ambayo hutakwa kwa kubadili sauti [th] katika Ki-Sanifu na kuwa sauti [s] katika Ki-Micheweni kama vile wazungumzaji wa Ki-Micheweni hutamka neno *samani* katika lahaja yao ikiwa katika Ki-Sanifu hutamka *thamani*. Vile vile katika neno sawabu ambalo hutamkwa na wazungumzaji wa Ki-Micheweni neno hilo hilo hutamkwa thawabu kwa wazungumzaji wa Ki-Sanifu. Ikiwa hiyo ni mionganini mwa tofauti inayojitikeza katika badiliko la sauti/ugeuzaji wa kitamkwa.

4.3.15 Tofauti ya Mabadiliko ya Sauti [l] kuwa [ly]

Pia kuna tofauti nyingine inayojitokeza katika Ki-Sanifu na Ki-Micheweni, tofauti hiyo ni ile sauti [l] ambayo inatamkwa katika Ki-Sanifu lakini wasemaji wa Ki-Micheweni huitamka sauti hiyo kama [ly]. Mifano ifuatayo inathibitisha tofauti:

Jedwali la 4.26: Tofauti Ya Sauti [L] Kuwa [Ly]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kulya	Kula
Nylango	Mlango
Lyangu	Langu
Nvulyana	Mvulana

Chanzo: Data ya Uwandani 2016

Jadweli lililopo hapo linathibitisha kwamba kuna tofauti katika usemajji wa sauti [l] ambayo inatamkwa katika Ki-Sanifu sauti hiyo hiyo hutamkwa [ly] katika Ki-Micheweni. Katika tofauti hiyo ni kwamba sauti [l] ambayo ni kitambaza cha ufizi hutumiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu na ile ambayo inachopekwa kiyeyusho [y]

hutumiwa na wasemaji wa Ki-Micheweni. Mifano mingine ni kama vile: *nlyanawe* likiwa ni neon ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Miceweni lakini neon hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *mlanawe*. Vile vile neon *lyako* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neon hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *lako*. Hivyo kutokana na mifano hiyo ni wazi kwamba kuna tofauti ya badiliko la sauti [l] kuwa sauti [ly] ambalo hufanya wasemaji wa Ki-Micheweni hutofautiana matamshi yao na wale wa Ki-Sanifu.

4.3.16 Tofauti ya mabadiliko ya Sauti [j]: [Ø]

Kuna tofauti nyingine katika utamkaji wa sauti [j] baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Kwa baadhi ya maneno. Hali hii inaonekana kuitia wasemaji wa Ki-Micheweni ambapo huibadilsha sauti [j] na kuidondosha katika baadhi ya maneno. Mifano ifuatayo inaweka bayana.

Jedwali la 4.27: Tofauti Ya Sauti [J] Kuwa [Ø]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Ifya	Jifya
Ipu	Jipu
Ipya	Jipyा
Iwe	Jiwe
Ivu	Jivu

Chanzo: data za Uwandani 2016

Katika mifano hiyo tunaona kuwa sauti [j], ambayo ni kizuio kwamizi ghuna cha ufizi, hutumiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu lakini sauti hiyo hudondoshwa na

wasemaji wa Ki-Micheweni. Hali hiyo hutokana na uzuiaji wa ukwamizi kwa baadhi ya maneno yaliyoanza sauti [j]. Kwa mfano, maneno hayo yalitarajiwa yachukue sauti [z] lakini hapo imedondoshwa. Kama vile katika neno *ipuni* neno linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni ila neno hilo linapoyumiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *jipu*. Vile vile neno *ivu* ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni nenohilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu huliyamka *jivu*. Sababu ya kutokea hali hii ni kwamba mashina au mizizi ya maneno hayo huanzia na sauti ambazo zina sifa ya [+anteria, -korona].

4.3.17 Tofauti za ukaakaishaji wa sauti

Ukaakaishaji ni utamkaji wa sauti ambao sehemu ya mbele ya ulimi husukumwa nyuma kuelekea kwenye kaakaa (Massamba, 20040) imenukuliwa na Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugh. Ukaakaishaji hufanya sauti isiyo ya kaakaa gumu kutamkwa katika uelekeo wa kaakaa gumu. Kwa kweli hii ni tofauti nyingine za kifonolojia baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu tunaziona katika ukaakaishaji. Mifano ifuatayo inaweka bayana:

Jedwali la 4.28: Tofauti Za Ukaakaishaji Bainya Ki-Micheweni Na Ki-

Sanifu

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Kyeupe	Cheupe
Kyungu	Chungu
Kyangu	Changu
Kyuo	Chuo
Kyama	Chama

Chanzo: Data ya Uwandani 2016

Katika mifano tulioiona hapo, sauti [ch] ambayo ni kikwamizwa kisoghuna cha kaakaa gumu hutamkwa hivyo hivyo katika Ki-Sanifu ila kwa upande wa waswmaji wa Ki-Micheweni sauthiyo huitamka [ly] ambayo ni kizuiwa kwamizi kisoghuna cha kaakaa laini. Mifano mingine tuyoweza kuiona ambayo inatofautisha sauti hizo ni kama vile: *kyandarua* ikiwa ni neno ambalo hutamkwa katika Ki-Micheweni lakini neon hilo linapotamkwa katika Ki-Sanifu hutamkwa *chandarua*, vile vile neno *kyama* ambalo hutamkwa wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *chamaHivyo* basi mifano iliyopo kwenye jadweli hilo inaweka bayana ya tofauti ya matamshi yanayotokana na kubadilika kwa sauti [ch] inayotumika katika Ki-Sanifu na kutamkwa [ky] katika Ki-Micheweni.

4.3.18 Tofauti za Udondoshaji wa Udondoshaji wa irabu/fonimu

Kwa mujibu wa Matinde (2012), Mgullu (1999) wanazumgumza kuhusu suala zima la udondoshaji kwamba ni kuacha baadhi ya herufi katika neno. Katika lugha ya Kiswahili baadhi ya lahaja katika matamshi yao huacha baadhi ya vitamkwa jambo ambalo hutofautiana katikautamkaji wa maneno hayo na kuathiri umbo la neno bila kuathiri maana halisi ya neno hilo. Wasemaji wa Ki-Micheweni baadhi maneno hudondoshwa sauti au vitamkwa kwa wasemaji hao ila kwa wasemaji wa Ki-Sanifu hawadondoshi kwa msamiati kama huo. Mifano inayoonekana katika jedwali la 4.29 inadhihirisha hoja hii.

Jedwali la 4.29: Udondoshaji Wa Irabu/Fonimu

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Uyu	Huyu
Awa	Hawa
Ii	Hi
Suzu	Siuzi
Wete	Waite
Hafla	Ghafla
Ika/eka	Weka
Hendi	Haendi
Ngia	Ingia

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Katika mifano tulioiona hapo inaonesha kwamba baadhi ya wasemaji wa Ki-Micheweni wanadondsha baadhi ya vitamkwa wakati wanapozungumza ingawaje wale wazungumzaji wa Ki-Sanifu hutamka maneno hayo kama yalivyo. Mifano iliyopo hapo inabainisha kwamba baadhi ya fonimu au irabu zinazopatikana katika Ki-Sanifu zinadondoshwa na watamkaji wa baadhi ya maneno katika Ki-Micheweni, neno *izi* ambalo hutamkwa na wazungumzaji wa Ki-Micheweni limedondosha sauti [h] wakati wale ambao wanazungumza Ki-Sanifu hulitamka neno hilo kama lilivyo (hizi) bila kudondosha kitamkwa. Vile vile katika neno *suzu* ambalo hutamkwa nawasemaji wa Ki-Micheweni limedondoshwa irabu [i] ambapo neno hilo hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hulitamka *siuzi* Ingawa tumebainisha msamiati ambao baadhi ya sauti zimedondoshwa katika baadhi ya maneno lakini tofauti hizo hazioneishi athari katika maana ya maneno hayo.

Wasemaji wa Ki-Micheweni baadhi ya maneno hudondosha irabu moja kunapokuwa na mfuatano wa irabu mbili na kuacha irabu moja, hivyo hivyo katika viwakilishi vioneshi pamoja na vivumishi vioneshi wasemaji wa Ki-Micheweni hudondosha kitamkwa [h]. Hata hivyo lengo hasa ni kuweza kubainisha namna utamkaji wa msamiati wa Ki-Micheweni unavyotofautiana na Ki-Sanifu.

4.3.19 Tofauti katika Uchopekaji

Baadhi ya fonimu huchopekwa wakati wazungumzaji wa Ki-Micheweni wanapozungumzaingawa katika Ki-Sanifu maneno hay ohayo yanakuwa hayana uchopekaji. Mfano wa maneno hayo tuyaaangalie katika jedwali lifuatalo.

Jedwali La 4.30: Tofauti Katika Uchopekaji[Y]

KIMICHEWENI	KI-SANIFU	Sauti iliyochopekwa.
Kiyazi	Kiazi	[y]
Kiliyo	Kilio	[y]
Ingiya	Ingia	[y]
Eneya	Anea	[y]
Mwambiya	Mwambia	[y]
Tembeya	Tembea	[y]

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Katika mifano hiyo tunaweza kusema kwamba uchopekaji umeweza kuonekana kupitia maneno ya kawaida yanayotimwa na wazungumzaji wa Ki-Micheweni jambo ambalo halikutendeka katika Ki-Sanifu. Uchopekaji huu umeweza kujitokeza kupitia maneno ambayo yanamfuatano wa irabu unganifu kama vile [i,a], [i,o], [e,a],

na kugeuka na kuwa kiyeyusho[y], mfano: linalotumiwa na wazungumzaji wa Ki-Michweni limechopekwa kiyeyusho [y] nenoingiyawakati neno hilo linapotumiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamkaingia . Vile vile neno *tembeya* limechopekwa kiyeyusho[y] lakini neno hilo linapotamkwa katika Ki-Sanifu hulitamka neno hilo kwa *tembea*. Uchopekaji huu umejitokeza pale ambapo irabu mbili zilijitokeza na iwapo irabu mbele [i,e] imekutana na irabu nyuma [o,u] au irabu chini[a]. Hivyo uchopekaji ni moja kati ya athari zinazopelekea mawasiliano au matamshi ya Ki-Sanifu kuweza kutofautiana na yale ya Ki-Micheweni kwa kuweka mifano bayana inayoonesha matamshi ya pande zote mbili.Pia kuna uchopekaji wa kiyeyusho [w] kwa watak maji wa Ki-sanifu na wale wa Ki-sanifu. Wasemaji wa Ki-Micheweni huchopeka kiyeyusho [w] katika maneno yenyenye mfuatano wa irabu mbili jambo ambalo halifanywi na watamkaji wa Kisanifu. Tuangalie mifano ifuatayo:

Jedwali 4.31 Tofauti katika Uchopekaji [w]

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU	KILICHOCHOPEKWA
Zowezi	Zoezi	[w]
Kujihashuwa	Kujihashua/ shaua	[w]
Teguwa	Tegua	[w]
Ubawo	Ubaο	[w]
Owa	Oa	[w]
Hashuwo	Hashuo	[w]
Uwa	Ua	[w]

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Mifano ilioonekana hapo inaonesha kwamba kama ilivyo katka mifano ya 21kwamba uchopeji umejitokeza kupitia maneno yenyе mfuatano wa irabu, hivyo basi katika Ki-sanifu hali hii hainekani kwa baadhi ya maneno kama haya. Mfano neno *ubawo* ni neno linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni ambalo limechopekwa kiyeyusho [w] neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka neno hilo *ubao*. Vile vile neno *owa* ambalo ni neno ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka *oa*. Tofauti hiyo ni ile ya uchopekaji wa kiyeyusho [w] kwa baadhi ya maneno kama ambavyo tumebainisha.

4.3.20 Tofauti Inayojitikeza katika Mpumuo

Mpumuo ni pumzi kali inayojitokeza wakati baadhi ya vitamkwa vinapotamkwa. *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lughha* (1990). Katika Ki-Micheweni baadhi ya sauti zinatamkwa hali kuwa zikiwa na mpumuo jambo ambalo halifanyiki katika Ki-Sanifu. Sauti ambazo kwa kawaida huwa na mpumuo zinapotamkwa katika Ki-Micheweni ni kama vile vitamkwa **p, k, t, na ch**. Matumizi haya ya mpumuo ni tofauti nyingine inayojitikeza katika msamati wa Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.

Tuangalie mifano ifuatayo:

Jedwali LA 4. 32: Tofauti katika Mpumuo

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU	UFAFANUZI
k ^h amba	Kamba	Uzi uliosokotwa
K ^h ata	Kata	Kitendo cha kutenganisha
Kit ^h u	Kitu	Jambo

Chanzo: Data ya Uwandani 2016

Mifano tulioiona hapo inadhihirisha kwamba kuna tofauti ya matumizi ya mpumuo kwa baadhi ya maneno baina ua Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Tofauti hii inaonekana kupitia maneno yaliyopo hapo kama vile kit^hu neno ambalo huwekwa mpumuo na wasemaji wa Ki-Micheweni lakini halina mpumuo neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu. Hali hii inaonesha kuwa ingawa tofauti ni za utamkaji tu wa maneno lakini maana ya maneno hayo yanakuwa ni sawa kwa viswahili hivyo viwili.

4.3.21 Tofauti za Mifuatano ya Irabu

Katika utafiti huu uchambuzi umegundua kuna tofauti nyingine ya mifuatano wa irabu baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.t Tofauti hii inajitokeza pale ambapo irabu mbili zitafuatana, zinapotokea hivyo katika Ki-Sanifu hutamkwa kama zilivyo ila kwa upande wa Ki-Micheweni irabu moja hudondoshwa na kutamkwa moja. Tuangalie mifano ifuatayo katika jedwali.

Jedwali LA 4 .33 Tofauti Katika Mfuatano wa Irabu

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU	IRABU
Suzu	Siuzi	i + u
Ningie	Niingie	i + i
Hendi	Haendi	a + e
Nambia	Niambia	i + a
Kuza	Kuuza	u + u

Chanzo data za uwandani

Katika mifano hiyo, tunaona kuwa irabu mbili zinapofuatana, hutokea mabadiliko katika utamkaji kwa wale wasemaji wa Ki-Sanifu kwa kutamka irabu moja na

nyengine kuidondosha ingawa kwa wasemaji wa Ki-Sanifu hutamka hivyo hivyo. Mfano katika neno haendi linalotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu lakini neno hilo hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hulitamka neno hilo kama hendi ambapo irabu moja imedondoshwa na kutamka irabu moja. Vile vile neno waite , ambalo linatamkwa na wasemaji wa K/S neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa K/M hutamkwa wete. Tofauti hiyo ya mfuatano inayojitokeza katika mfuatano wa irabu inaathiri matamshi pekee bila kuathiri maana ya maneno hayo. Kwa maana hiyo maneno hayo yanatofautiana kimatamshi ila maana yanakuwa sawa.

4.3.22 Tofauti za Maneno yenye Kuambatana

Katika utumiaji wa baadhi ya maneno yaliyoundwa kutokana na njia hii ya miambatano baina watamkaji wa Ki-Sanifu hutofautiana wakati wa utamkaji wa maneno hayo na wale wa Ki-Micheweni. Kwa wale wazungumzaji wa K/S wanapotamka maneno hayo huyatamka katika hali ya kuyaunganisha lakini wasemaji wa K/M huyatamka maneno yakiwa neno moja na neno jingine ambalo ni ambatano hulidondosha.

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Hoho	Pilipipihoho
Nyungwi	Nyungunyungu
Sheli	Shelisheli
Kipure	Kipurepure
Boko	Bokoboko
Yungi	Yungiyungi

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Mifano iliyopo hapo inaonesha kwamba wazungumzaji wa Ki-Sanifu hutumi maneno ambatono kwa baadhi ya maneno lakini kwa wale ambao ni wasemaji wa Ki-Micheweni hudondosha neno moja na kutamka neno moja. Mfano huu unaonekana kupitia neno *nyungunyungu* kwa wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka neno hilo katika hali ya kuliambatanisha wakati kwa wasemaji wa Ki-Micheweni hulitamka neno ho kwa kulidondosha neno moja yaani hulitamka *nyungwi*. Mfano mwengine ni sheli ambalo hutamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni linapotamkwa neno hilo na wasemaji wa Ki-Sanifu hulitamka neno hilo shelisheli. Hata hivyo ingawa maneno hayo yamedondoshwa neno moja lakini haikuathiri maana kwa wazungumzaji wa KI-Micheweni na wale wa Ki-Sanifu.

4.3.23 Tofauti Zinazojitokeza katika Maneno ya Urudufishaji

Kuna tofauti nydingine ya maneno ya kurudia rudia kwa wasemaji wa Ki-Micheweni na wale wa Ki-Sanifu ambapo baadhi maneno ambayo nay a kurudia rudia wasemaji wa Ki-Micheweni huyatamka maneno hayo bila kuyarejea kama ambavyo yanatamkwa katika Ki-Sanifu. Tofauti huwafanya wasemaji wa Ki-Micheweni katika matumizi yao ya msamiati hawatumii urudufishaji kwa baadhi ya maneno na wale wasemaji wa Ki-Sanifu huyatamka maneno ya urudufishaji kama yalivyo katika matumizi yao ya msamiati. Tuangalie mifano ifuatayo:

Jedwali LA 4.35: Tofauti ya Maneno ya Urudufishaji

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
Sheli	Shelisheli
Yungi	Yungiyungi
Boko	Bokoboko
Nyungwi	Nyungunyungu

Chanzo: Data za uwandani 2016

Maneno yaliyopo hapo yanabainisha kuwa katika Ki-Sanifu baadhi ya maneno yanakuwa na urudufishaji ambapo wazungumzaji wa Ki-Micheweni hawana tabia ya kurudia neno au sehemu ya neno. Kwa mfano neno kama vile *sheli sheli* ni neno linaloonesha kurudiwa na wasemaji wa Ki-Sanifu ingawa neno hili linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni hutamkwa *sheli*. Vile vile, neo *bokobokoni* neno ambalo linatamkwa na wasemaji wanaotumia Ki-Sanifu lakini neno hilo hilo linapotamkwa na wazungumzaji wa Ki-Micheweni hutamkwa *boko*. Katika maelezo na mifano ya maneno hayo tumebaini kwamba kuna urudiaji wa baadhi ya maneno kwa watamkaji wa Ki-Sanifu na wale ambao wanazungumza Ki-Micheweni hakuna tabia hiyo ya urudiaji wa maneno, mara nyingi urudiaji wa maneno hayo hutokea kwenye nomino kama ambavyo tumeona baadhi ya mifano. Hivyo hali hii imebainisha kwamba kuna tofauti za msamiati baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.

4.3.24 Tofauti Zinazotokana na Lafudhi

Massamba na wenzake (2004) wanazungumza kuhusu lafudhi kwa kusema kwamba lafudhi ni sifa ya kimasukizi inayohusiana na kusikika kwa sauti wakati wa kutamka

matamshi ya mtu binafsi ambayo humpa msemaji utambulisho fulani ama kijamii au kieneo. Hali hii ina maana kwamba mazingira ya mtu yawe ya kijamii au kijiografia yanaweza kuleta athari za lafudhi kwa wasemaji wa Ki-Micheweni na wale wa Ki-Sanifu. Mtu yejote hutambulikana wapi anapotoka kutokana na lafudhi yake, kwani wazungumzaji huathiriwa na mazingira yao ya kijiografia kama ambavyo wasemaji wa Ki-Micheweni walivyoathiriwa na mazingira yao na kusababisha kuwepo tofauti ya utamkaji baina yao na wale wa Ki-Sanifu. Tuangalie mifano ifuatayo inavyobainisha ukweli huo.

Jedwali LA 4.36 Tofauti Zinazotokana na Lafudhi

KI-MICHEWENI	KI-SANIFU.
Kiza	Kiambaza
Magovi	Mataka
Kyakwe	Chake
Hilino	Hilo hapo
Tari	Dufu
Vipuji	Vidimbwi
Gurubi	Kozi
Alisa	Ugua
Rasite	Barabara
Machama	Mataka
Ngovi	Ngozi

Chanzo: Data za Uwandani 2016

Mifano iliyopo hapo inatambulisha kwamba kuna tofauti za utamkaji wa maneno kwa wasemaji wa Ki-Micheweni na wale wa Ki-Sanifu. Tofauti hiyo ni ile inayotokana na mazingira wanayoishi wasemaji wa Ki-Micheweni huathiri usemajii katika viswahili hivyo viwili. Usemajii huu unawatambulisha wazungumzaji wanaoishi eneo hilo kuweza kujulikana na wazungumzaji wa maeneo mengine. Mfano neno *hilino / hilyo* ni maneno yanye maana moja ambayo yanatamkwa na wasemaji wa Ki-Micheweni jambo ambalo neno hilo linapotamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu hutamkwa *hilo hapo*. Hii ina maana kwamba maeneo mengine pia hutofautina kilafudhi namaeneo mbali mbali yaliyomo katika kisiwa cha Pemba.

4.4 Matokeo ya Utafiti

Matokeo ya utafiti huu yanaonesha kwamba kuna tofauti nyingi za msamiati katika Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu. Tofauti hizo zinalezwa hapa kulingana na kufuata malengo mahsusini ya utafiti huu.

4.4.1 Tofauti za Msamiati Unaohusu Shughuli za Kilimo Unaotofautina baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu

Hata hivyo utafiti huu umegundua kuwa katika shughuli mbali mbali za kilimo msamiati wake kwa kiasi kikubwa unatofautiana kimatamshi baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu. Data iliyokusanywa imethibitisha na kubainisha tofauti hiyo ya matamshi katika viswahili hivyo viwili, licha ya kuwa maana inayowakilisha katika msamiati huo yanabaki kuwa sawa Jumla ya maneno 210 yalichunguzwa na kuonesha kwamba ili kulifikia lengo maneno hayo yalionesha kuna tofauti ya matamshi kati ya Kiswahili kinachozungumzwa Micheweni na kile cha Kiswahili sanifu.

4.4.2 Tofauti ya Msamiati wa Nyumbani, Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu

Vile vile uchunguzi wa utafiti huu umegundua kuna tofauti za utamkaji wa msamiati unaohusu mazingira ya nyumbani baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu, jambo ambalo tofauti hizo zinafanya wale wasiokuwa wakaazi wa eneo hilo kutopata maana halisi ya msamiati unaotamkwa. Tofauti hizo zilijikita zaidi katika upande wa matamshi lakini pia hata baadhi ya maneno yameonesha maumbo ya maneno hayo yamechangia katika kuleta tofauti za msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu. Katika kulifikasi lengo hili maneno 72 yalionesha kuwa ni uthibitisho wa tofauti ya msamiati baina ya viswahili hivyo.

4.2.3 Athari za Kimawasiliano za Fonolojia Msamiati wa Kiswahili Sanifu na Kimicheweni


Aidha utafiti huu umegundua kwamba kuna athari mbali mbali za kifonolojia ambazo hutokea katika matamshi ya Kiswahili cha Micheweni zinazotofautiana na Kiswahili Sanifu. Athari hizo ni nyingi miongoni mwa hizo ni mabadiliko ya sauti, udondoshaji wa sauti, uchopekaji wa sauti na nyenginezo. Utafiti uligundua kwamba jumla ya maneno 120 yalionesha tofauti zitokanazo na athari za kimawasiliano katika fonolojia zinazotofautisha Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu.

Kiujumla tofauti zote ambazo zimegunduliwa katika msamiati huu uanonesha tofauti mbali mbali za matamshi lakini pia ndani ya matamshi hayo yanaonesha maumbo ya maneno yamaneno yamechangia kutofautisha Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu.

4.3 Muhtasari wa Sura

Sura hii imeweza kubainisha tofauti za msamiati baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu ambazo hupelekea kuwepo tofauti ya matamshikwa viswahili hivyo viwili.Tofauti hizo tumeweza kuziona kupitia msamiati unaohusiana na shughuli mbali mbali za uvuvi, msamiati unaohusiana na shuhuli za kilimo pamoja na msamiati ambao hutumika katika mazigira ya nyumbani.

Vile vle tumeweza kubaini athari za kifonolojia ambazo zinafanya viswahili hivi viwili kuwa tofauti yaani Ki-Sanifu na Ki-Micheweni. Tumegundua kwamba athari hizo ziko nyingi ila mionganini mwao ni kama hizo tuliozifafanua na kuweza kuthibitisha kwamba katika fonolojia ya Ki-micheweni inaweza kusababisha kutokea kwa tofauti za kiuseaji au utamkaji katika Ki-Sanifu.Tofauti hizo ni kama vile mabadiliko ya sauti m.f. sauti [m] kuwa sauti [n] katika Ki-Micheweni, [dh] Ki-Sanifu kuwa [z] Ki-Micheweni, udondoshaji wa baadhi ya vitamkwa, ukaakaishaji,n.k. kulingana na mjadala mrefu pamoja na mifano hiyo tumebaini kwamba ziko tofati nyindi za kiusemajji au kimatamshi zinazotokana naathari za Kifonolojia ambazo hufanya matamshi ya Ki-Sanifu kuwa tofauti katika matashi tu inawa maana yanakuwa yaleyale



SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPEDEKEZO

5.0 Utangulizi

Utafiti huu ulijkita katika kuangalia mada kuu iliyosema tofauti za matamshi baina Kiswahili kizungumzwacho Micheweni na Kiswahili sanifu ambacho kinatoka katika kisiwa cha Pemba. Katika utafiti huu mengi yaliweza kupatikana ambayo yalihusiana na tofauti za msamiati unaozungumzwa na Ki-Micheweni na Ki-Sanifu .tutakachoangalia zaidi katika sura hii ni muhtasari wa wa matokeo ya kazi hii, hitimisho lake na mapendekezokuhusu tafiti zijazokatika Ki-Micheweni na Ki-Sanifu.

5.1 Muhtasari wa Utafiti

Kwa ujumla utafiti huu ulikuwa na lengo kuchunguza msamiati wa Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu ili kubaini tofauti mbali mbali za matamshi kuitia msamiati wake zinavyotofautiana. Utafiti huu ulifanywa katika Kisiwa cha Pemba, wilaya ya Micheweni na kuhusisha wakazi wa vijiji vilivyomo ndani ya Micheweni kama vile Kiuyu- mbuyuni, Micheweni chamboni na Shumba mjini. Walengwa walioshiriki katika utafiti huu katika kujaza dodoso na usaili walikuwa ni 60, ambao waliishi mzingira ya Micheweni ikiwa ni wazee wenye umri kati ya miaka 45-70. Ambao kwa kiasi kikubwa hawajaathiriwa na Ki-Sanifu na hawajapata pia athari za maendeleo ya sayansi na teknolojia. Katika kufikia lengo kuu la utafiti huu ambalo ni kuchunguza mahusiano ya tofauti baina ya misamiati ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu na jinsi tofauti hizo zinavyoathiri mawasiliano baina ya wazungumzaji wa lugha hizo, utafiti huu ulikuwa na malengo mahsusini yafuatayo:

- i. Kubainisha misamiati ya lahaja ya Kipemba cha Micheweni itokanayo shughuli za kilimo pamoja na mazingira ya nyumbani.
- ii. Kubainisha misamiati ya Kiswahili sanifu.
- iii. Kubainisha athari za kimawasiliano zitokanazo na kifanoljiazinazofautisha msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili sanifu.

Madhumuni hayo yakiwa ndiyo ya msingi yaliyojenga utafiti huu katika kuyafikia malego, mtafiti aliandaa pamoja na kutumia maswali ambayo ni mwongozo wa usaili na pia alitumia dodoso kwa kuwatemebelea washiriki wa utafiti huu ambapo walitakiwa kutaja vibadala vya maneno waliyopangina kulingana na yanavyotumika katika maeneo husika wanamoishi.

Katika kubainisha tofauti hizi za msamiati mjadala huu umefanywa kwa kutumia nadharia ya Isimu linganishi. Imetumika nadharia hii ili kuweza kulinganisha na kulinganua kipengele hiki kilichokusudiwa kama ambavyo utafiti wetu unatuelakaza. Katika kuibua tofauti mbali mbali za matamshi vigezo viwili tuliviangalia ili kuchambua maneno pamoja na matini mabali mbali zilizokusanywa uwandani. Kwanza tulichunguza msamiati wa msingi ambao anahu shughuli mbali mbali za kilimo zinazopatikana katika maeneo wanamoishiwasemaji wa Ki-Micheweni..Pia tukachunguza msamiati ambao ni wa mazingira ya nyumbani ambao wasemaji wa viswahili hivi viwili wanatofautianakimatamshi na baadhi ya maneno yanatofautiana hata maumbo.

Kipengele cha pili tulichoangalia ni kile ambacho kinaonesha athari za kifonolojia zitokanazo na matamshi ya Ki-Micheweni yakitofautiana na Ki-Sanifu. Katika

kubainisha vipengele hivyo mtafiti aligundua kwamba ingawa kuna tofauti mbali mbali za matamshi ya msamiati baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu lakini maana ya maneno hayo yalioneckana yana maana sawa kwa pande zote mbili. Ama kwa upande mwengine, utafiti huu umepangwa kwa sura tano, sura ya kwanza imejengeka kwa vipengele mbali mbali kama vile: utangulizi, usuli wa tatizo, tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, mawanda ya utafiti, umuhimu wa utafiti pamoja na vikwazo vyta ya utafiti na utatuzi wake na mwisho nihitimisho la sura hii.

Sura ya pili ya utafiti huu inahusiana na mapitio ya kazi tangulizi ambayo inajumuisha kazi mbali mbali tangulizi zilizofznywa na watafiti waliopita, mkabala wa kinadharia ambao umejadili kiunzi cha nadharia itakayotumika katika utafiti huu ikiwa ni nadharia ya Isimu Linganishi na hitimisho la sura.

Sura ya tatu inaelekeza mbinu pamoja na njia za utafiti ikiwa ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, watoa taarifa, usampulishaji, vifaa vyta ya utafiti, ukusanyaji data, mkabala wa kimaadili, uchambuzi wa data, mpangilio wa utafiti na hitimisho la sura.

Katika sura ya nne ya utafiti huu inahusiana na uwasilishaji na uchambuzi wa data zilizokusanywa kutoka kwa watafitiwa ikifuatiwa na sura ya tano ambayo imetoea muhtasari wa matokeo ya utafiti, hitimisho na mapendekezo ya tafiti zitakazofanywa baadae.

5.2 Hitimisho

Utafiti huu umelinganisha msamiati baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu kwa kufuata misingi ya nadharia ya isimu linganishi. Hata hivyo, utafiti huu umejaribu kuonesha hatua mbali mbali zinazotofautisha msamiati wa Kiswahili cha Michewweni na Kiswahili Sanifu. Kupitia shughuli abali mbali zikiwemo za kilimo, uvuvi, pamoja na mazingira ya nyumbani vimeangalia tofauti ya msamiati baina ya viswahili hivyo.

Kwa ujumla utafiti huu umebainisha athari za mawasilino hayo zinazoatikana katika fonolojia ya matamshi na msamiati mbali mbali wa viswahili hivyo. Hivyo, iingawa kuna tofauti katika msamiati huo lakini pia kuna mfanano ambao kwa kiasi kubwa msamiati huo unafanana kimaana. Hapa ni kwamba maana ya msamiati unaozungumzwa na wasemaji wa Ki-Micheweni unafanana kimaana na ule ambao unatamkwa na wasemaji wa Ki-Sanifu.

Adha kulingana utafiti huu kuna maswali mbali mbali ambayo napaswa kujiuliza kama vile, ni kwa sababu gani Kiswahili cha Mi-Micheweni kinatofautiana sana na Kiswahili Sanifu? Je tofauti hizo zinaweza kubainishwa katika vipengele vingine kamavile muundo, mtindo na maana? Jee ni kweli kwamba Ki-Micheweni kinaweza kutofautiana na maeneo mengine ya pemba? Kwa kudhihirika maswali kama hayo ni wazi kuwa bado tafiti nyingine zinahitajika ili kubainisha sababu mbali mbali za tofauti hizo.

5.3 Mapendekezo

Utafiti wowote ule unaweza kuwa haukujitoshelezana kumaliza kila kitu katika eneo linaloshughulikiwa. Hivyo basi tunaiweka kazi hii katika hatua ya mwanzo ya kuzielekea kazi nyingine pamoja na kuzitafuta tofauti za kiisimu baina ya Ki-Micheweni na Ki-Sanifu. Nimapendekezo yetu kwamba utafiti zaidi ufanywe ambao utahusu kulinganisha vipengele vingine vya matumizi ya lugha vikiwemo maumbo ya maneno yavyotofautiana baina ya Kiswahili cha Micheweni na Kiswahili Sanifu.

Adha tunapenda utafiti ufanywe ambao utazingatia maeneo kwa kuchunguza tofauti za msamiati kutoka eneo moja na jingine ndani ya Kisiwa cha Pemba atakaotumia nadharia nyingine.

Pia, tanasisitiza kwamba maeneo ya vijijini yatiliwe mkazo katika kufanya utafiti ili kuona tofauti mbambali zinazojitokeza kutoka kijiji kimoja na kijiji kingine badala ya kueka mkazo zaidi maeneo ya mjini.

BIBLIOGRAFIA

- Anttila, R. (1972). *An Introduction to Historical and Comparative Linguistics*. New York: Macmillan Publishing Co. Inc.
- Batibo, H. M. (1982). *Mawazo ya Mwanzo kuhusu Uhusiano wa Lahaja za Kiswahili za Kusini* (Makala ya Semina). Chuo Kikuu cha Dar es salaam
- Ingrams, W. H (1924). “The Dialects of the Zanzibar Sultanate.” In Bulletin of the School of Oriental and African Studies, Vol.III, Part III, London, pp 533-550.
- Khamis, S. A. M. (1984). “Urban Versus Rural Swahili; A Study of Pemba Varieties.” (Tasnifu ya uzamivu, haijachapishwa) Karl Marx University, Leipzig.
- Kipacha, A. (2003). *Lahaja za Kiswahili*. Dar es Salaam: KIUTA.
- Kothari, C. R (2004). *Research Methodology: Methods and Techniques*. New Delhi: New Age International (P).
- Mdee, S. J (2014), OSW 613: “Isimu Jamii,” (hakijachapishwa), Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.
- Massamba, D. P. B. (2002). *Historia ya Kiswahili: 50BK hadi 1500BK*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Massamba, D. P. B. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lughya*. Dar es Salaam: TUKI.

- Mathooko, P. M. (2007). *Isimu Jamii: Misingi na Nadharia*. Nairobi: Njiku Books.
- Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lughaa: Isimu na Nadharia*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Mgullu, R. S. (2001) *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Msanjila, Y. P., Kihore, Y. & Massamba, D. P. B. (2009), *Isimu Jamii: Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mshindo, H. B. (1989). “The Use of ‘KA’ in Pemba Swahili Variety.” Unpublished M.A Linguistics of The University of Dar es Salaam.
- Polome, E. C. (1967). *Swahili Language Handbook*, Center of Applied Linguistics, Washington DC.
- Saucleux, C. (1909). *Grammaire des Dialectes Swahili*, Paris.
- Temu, C. (1980). *Lahaja za Kiswahili: Ripoti ya Utafiti*, Dar es Salaam: TUKI.
- TUKI (2004) *Kamusi Ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI.
- Whiteley, W. H. (1958). *The Dialects and Verse of Pemba*. Inter-territorial Language (Swahili) Committee
- www.katoa.net.nz/kaupapa_maori /kaupapa.maori_ethics at 8:53 am.

VIAMBATANISHO

KIAMBATANISHO NO 1: Orodha ya Msamiati wa Nomino

s/no.	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
1.	Kituwa	Kichaka
2.	Kijingwi	Kijembe kidogo cha mkono
3.	Ugwe	Kamba
4.	Gurubi	Kozi/gubi
5.	Kyuwo	Chuo
6.	Guwa	Sehemu iliyolimwa ikaachwa
7.	Chale	Sehemu iliyolimwa
8.	Mbeu	Mbegu
9.	Chepe	Tambara
10.	Chanjaa	Sehemu isiyolimwa
11.	Book	Bokoboko
12.	Pindi	Tambara
13.	Pukusa	Pukusi
14.	Ngwe	Sehemu utakayolima
15.	Mrashi	Mchaichai
16.	Mishonga	Majimbi
17.	Duta	Mwinuko
18.	Kichuguu	Kilima
19.	Mboga ya viazi	Mtoriro/ mriba.
20.	Muingajini	Mpambawake
21.	Kivumbasi	Kivumbani
22.	Nkundenyika	Mkunde
23.	Kikwayakwaya	Mboga
24.	Hoho	Pilipili hoho
25.	Peku	Ungo
26.	Senti	Sinia
27.	Nkanshi	Kijiko cha mchuzi

s/no.	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
28.	Nchamo	Mkeka mbovu
29.	Shana	Shana
30.	Dishi	Sufuria
31.	Kibia	Chungu
32.	Kibati	Kibakuli
33.	Kiza	kiambaza
34.	Kocho	Panya
35.	Ifya	Jifya
36.	Upenu	Pembezoni mwa nyumba
37.	Ubungu	Uwanja
38.	Kati	Chumbani
39.	Bandani	Ukumbini
40.	Kiza	kiambaza
41.	Kyumba	Chumba
42.	Kyama	Chama
43.	Kyungu	Chungu
44.	Kiwete	Mlemavu
45.	Kekefu	Kwikwi
46.	Pumbu	Busha
47.	Tango	Boga
48.	Nyonga	Maradhi ya mgongo
49.	Ipu	Jipu
50.	Kipisi	Kiungulia
51.	Pele	Upele
52.	Kyombo	Chombo
53.	Buli	Birika
54.	Ndaza	Chichi
55.	Kijio	Chajio
56.	Vishuka	Chamchana

s/no.	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
57.	Besi	Beseni
58.	Unju	Asubuhi
59.	Badia	Bajia
60.	Nyange	Hariri
61.	Kurumbiza	Kurumbizi
62.	Ndudu masika	Kumbikumbi
63.	Kupa	Kupe
64.	Shawa	Chawa
65.	Nkazahau	Mke wa mjomba
66.	Wifi	Mke wa kaka
67.	Mame	Mama
68.	Dade	Dada
69.	Mamenkuu	Mamamkubwa
70.	Kake	Kaka
71.	Mameye	mamayake
72.	nshekwa	mchekwa
73.	Muamu	Shemegi
74.	Mendogo/mamendogo	Haloo/ mamamdogo
75.	Balehe	Balehe
76.	Shuhuli	Shughuli
77.	Horofa	Ghorofa
78.	Hafula	Ghafla
79.	Shindano	Sindano
80.	Shikio	Sikio
81.	Matushi	Matusi
82.	Shurua	Surua
83.	Mapota	Maziwa mabivu
84.	Mwiku	Uporo
85.	Zarau	Dharau

s/no.	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
86.	Zahabu	Dhahabu
87.	Azuhuri	Adhuhuri
88.	Hazira	Hadhira
89.	Hazarani	hadharani
90.	Nndefu	Mrefu
91.	Nndembo	Mrembo
92.	Nchele	Mchele
93.	Nkate	Mkate
94.	Nkeka	Mkekka
95.	Nkoba	Mkoba
96.	Sanli	Samli
97.	Zicho	Jicho
98.	Zino	Jino
99.	Zina	Jina
100.	Ziko	jiko
101.	Mwivi	Mwizi
102.	Ngovi	Ngozi
103.	Mjuvi	Mjuzi
104.	Mkwevi	Mkwezi
105.	Shaza	Chaza
106.	Shumvi	Chumvi
107.	Shawa	Chawa
108.	Shungwa	Chungwa
109.	Mpisi	Mpishi
110.	Mosi	Moshi
111.	Singo	Mshingo
112.	matapisi	matapishi
113.	Nlyango	Mlango
114.	Mvulyana	Mvulana

s/no.	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
115.	Samani	Thamani
116.	Sawabu	Thawabu
117.	Hanisi	Hanithi
118.	Hadisi	Hadithi
119.	Zowezi	Zoezi
120.	Owa	Oa
121.	Uwa	Ua
122.	Ubawo	Ubaو
123.	Kiyazi	Kiazi
124.	Kiliyo	Kilio
125.	Sheli	Shelisheli
126.	Yungi	Yungiyungi
127.	Nyungwi	Nyungunyungu
128.	Kamasi	Mafua
129.	Taka	Usaha
130.	Tari	Dufu
131.	Vipuji	Vidimbwi
132.	Tumbi	Pakacha
133.	Nndu	Panga
134.	Machama	Mataka
135.	Magovi	mataka

KIMBATANISHI NO II: Orodha ya Msamiati wa Vitenzi

S/NO	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
1.	Kukatia	Kulima jembe la kwanza
2.	Kuuwatiza	Kutoa mche na kuupanda sehemu nyingine
3.	Kuumbikia	Kupanda kabla ya mvua
4.	Kukatia	Kuunganisha madongo unapolima
5.	Kutema	kufyeka
6.	Kauku	Kaondoka
7.	Tongoa	Sema
8.	Kulya	Kula
9.	Dengue	popoa
10.	Chama	hama
11.	gwiya	kamata
12.	Dumua	kata
13.	Chamia	hamia
14.	Teguwa	Tegua
15.	Songa	Suka
16.	Sebu	Sitaki
17.	Hashuwa	Hashua/ shaua
18.	Mwambiya	Mwambia
19.	Ingiya	ingia
20.	Keleshi	Kaakitako
21.	Kwama	Fukuza

22.	Geleka	Potea
23.	Pisa	Unguza
24.	Penjewa	Furahi
25.	Chunza	Angalia
26.	Kuuya	Kurudi
27.	Kufisa	Kupeleka
28.	Bofya	Bonyeza
29.	Enza	Fuata
30.	Kucha	kuogopa
31.	Twaa	Chukua
32.	Kwaga	Potea
33.	Bauwa	Kojoa
34.	Alias	Uguza
35.	Gwiya	kamata
36.	Suzu	Siuzi
37.	Ningie	Niingiw
38.	Hendi	Haendi
39.	Kuza	kuuza
40.	Nambia	niambia
41.	Kat ^h a	kata

KIAMBATANISHO III: AINA NYENGINEZO ZA MSAMIATI

S/NO.	KI-MICHEWENI	KI-SANIFU
1.	Kyakwe	Chake
2.	Hilino	Hilo hapo
3.	Ani?	Nani?
4.	Vii?	Vipi?
5.	Waa?	Wapi?
6.	Kii?	Kipi?
7.	Nii?	Nini?
8.	Ngaa?	Ngapi?
9.	Kyangu	Changu
10.	Kidigi	Kidogo
11.	Kimbamba	Chembamba
12.	Hino	Hiyo
13.	Kyepeu	Chepesi
14.	Kyema	Kizuri
15.	Kyadanda	Chang'ara
16.	Kit ^h u	kitu
17.	Hebuvye	Hatakizake
18.	Kinyaa	Uchafu
19.	Kidiigi	Kidogo sana
20.	Kanliaaa	Amelia sana
21.	Mjeuuuri	Mjeuri sana

22.	Kifuuupi	Kifupi sana
23.	Hairi	Ghairi
24.	Hazarani	Hadharani
25.	Hafla	Ghafla
26.	Sawabu	Thawabu
27.	Salasini	Thelathini
28.	Lyangu	Langu
29.	Ipya	Jipyा
30.	Kyeupe	Cheupe
31.	Uyu	Huyu
32.	Ii	Hii
33.	Awa	Hawa
34.	Hashuwo	Hashuo

KIAMBATANISHO NO IV: HOJAJI KUHUSU TOFAUTI ZA MSAMIATI

Katika lugha ya Kiswahili tuna baadhi ya maneno ambayo yanaonekana yana vibadala vyake yanapotumiwa na watumiaji wengine. Vibadala hivyo huonenesha usawa katika maana, au huwa na maana inayokaribiana au maana hutofautiana kabisa. Katika orodha hii ya maneno naomba uandike maneno au istilahi au kifungu cha maneno mbadala kulingana na yanavyotumika katika jamii yako:

1. Kwa Kulinganisha Msamiati Unaohusu Shughuli za Kilimo

MSAMIATI	KIBADALA	MSAMIATI	KIBADALA
Kulima jembe la kwanza	Kamba
Pakacha	Kichaka
Kupanda miche	Kupanda kabla ya mvua
Kufyeka	Pahala pasijapolimwa
Pahala panapolimwa	Kidimbwi
Bokoboko	Pukusa
Sehemu utakayolima	Panga
Mtoriro	Kilima
Majimbi	Mchaichai
Gubi	Kivumbani
Mpamba wake	Mribaziwa
Mkunde	Boga
Pilipili hoho	Mastafeli
Embesakua	Ubuyu

2. Kulinganisha Msamiati Unaohusu Mazingira ya Nyumbani

MSAMIATI	KIBADALA	MSAMIATI	KIBADALA
Jifya	Kibakuli
Kibakuli	Chungu
Sufuria	Shanuo
Mkekä mbovu	Kijiko cha mchuzi
Sinia	Ungo mbovu
Uwanja	Pembezo mwa nyumba
Chumbani	Ukumbini
Chuo	Chumba
Mlemavu	Kwikwi
Busha	Maradhi ya mgongo
Jipu	Kiungulia
Mafua	Usaha
Upéle	Kaondoka
Sema/zungumza	Kula
Sitaki	Kaa kitako
Hama	Kata
Kuogopa	Uguza
Popoa	Suka
Fukuza	Potea

Unguza	Furahi
Angalia	Kurudi
Kupeleka	Bonyeza
Kojoa	Toa
Fuata	Chukua
Funga mlango	Fungua kufuli
Kupotea	Kanyaga
Chutama	Hujui
Haraka	Tupa
Angusha	Tapika
Suka ukili	Suka nywele
Chana nywele	Nani
Vipi?	Wapi?
Kipi?	Kipi?
Nini?	Ngapi?
Kurumbizi	Kumbikumbi
Hariri	Panya
Chawa	Mende
Mke wa mjomba	Mke wa kaka
Mama	Kaka
Dada	mamamkubwa
Shemegi	Chajio
Maziwa mabivu	Uporo

**KIAMBATANISHO NO V: JADWELI LA MWONGOZO WA USAILI WA
KUCHUNGUZA TOFAUTI ZA MSAMIATI ZINAZOTOKANA NA ATHARI
ZA KIFONOLOJIA**

Baadhi ya maneno yanayotumika katika Kiswahili sanifu yanakuwa ni tofauti na yanavyotumiwa katika maeneo mengine (huwa na vibadala vyake). Maneno hayo ingawa hutofaitiana kimsamiati lakini maana yake yanakuwa sawa, hukaribiana au hutofautiana kabisa. Katika orodha hii ya maneno naomba utaje maneno au istilahi au kifungu cha maneno mbadala yanavyotumika katika jamii yako.

MSAMIATI	KIBADALA	MSAMIATI	KIBADALA
Baleghe	Ghairi
Shughuli	Kughani
Ghorofa	Ghafla
Dhahabu	Fedha
Dharau	Adhuhuri
Hadharani	Mchele
Mkate	Mkoba
Samli	Mjomba
Mkeka	Jicho
Jina	Jiko
Jino	Mwizi
Ngozi	Mjuzi
Mkwezi	Nchi
Chawa	Chumvi
Mchekwa	Chungwa
Mpishi	Moshi
Shingo	Matapishi
Sindano	Sikio
Matusi	Sindikiza
Thamani	Hanithi

Thawabu	Thelathini
Hadithi	Kula
Mlango	Langu
Mvulana	Jifya
Jipu	Jiwe
Jivu	Cheupe
Chungu	Change
Chuo	Huyu
Hii	Hawa
Siuzi	Waite
Weka	Haendi
Ingia	Weka
Zoezi	Tegua
Ubaao	Oa
Hashuo	Ua
Kiazi	Enea
Kilio	Mwambia
Tembea	Siuzi
Niingie	Niambia
Haendi	Kuuza
Pilipili Hoho	Nyungunyungu
Shelisheli	Kipurepure
Bokoboko	Yungiyungi
Kiambaza	Mataka
Chake	Hilohapo
Dufu	Vidimbwi
Kozi	Uguza
Barabara	Ngozi

Ahsanteni sana kwa ushirikiano wenu